

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA UMMY A. MWALIMU  
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA  
2021/22



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, akisalimiana na Wananchi wa Kijiji cha Mkata Wilayani Handeni Mkoani Tanga, wakati wa ziara yake ya kikazi alipotembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo ya Wananchi

DODOMA

Aprili, 2021



**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Ummu A. Mwalimu (Mb) akizungumza na mtoto Bakari Chacha aliyekuwa amelazwa kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza wakati wa ziara yake ya kikazi Mkoani humo.**



Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, anayeshughulikia Elimu **Mhe. David E. Silinde (Mb)** akitoa maelekezo wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa bweni katika shule ya Sekondari Kitima Wilayani Tandahimba Mkoani Mtwara.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, anayeshughulikia Afya **Dkt. Festo Dugange (Mb)** akitoa maelekezo kwa Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Itulahumba Wilayani Wanging'ombe Mkoani Njombe wakati wa ziara yake ya kikazi Mkoani humo.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

## Viongozi Wakuu



**Mhe. Ummy A. Mwalimu (Mb)**  
Waziri wa Nchi OR- TAMISEMI



**Mhe. David E. Silinde (Mb)**  
Naibu Waziri OR- TAMISEMI



**Mhe. Dkt. Festo J. Dugange (Mb)**  
Naibu Waziri OR- TAMISEMI



**Prof. Riziki S. Shemdoe**  
Katibu Mkuu OR- TAMISEMI



**Dkt. Grace E. Magembe**  
Naibu Katibu Mkuu (AFYA)



**Gerald G. Mweli**  
Naibu Katibu Mkuu (ELIMU)

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS  
- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA,  
MHESHIMIWA UMMY ALLY MWALIMU (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA  
FEDHA 2021/22.**

**A. UTANGULIZI**

- 1. *Mheshimiwa Spika*,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, naomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2 na Mafungu 26 ya Mikoa

na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/22.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha tena kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.
3. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nampongeza **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia kauli mbiu yake ya “*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi Iendeleo*”, Watanzania wana Imani na matumaini makubwa nae na kuwa katika Awamu ya Sita nchi yetu itapiga hatua kubwa zaidi za kimaendeleo hususan katika nyanja za kiuchumi na kijamii na hivyo kuwanufaisha wananchi walio wengi na hasa wanyonge.
4. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe pole zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, kwa msiba mkubwa kwa Taifa letu kwa kuondokewa na mpendwa wetu na kipenzi cha Watanzania Hayati **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeaga dunia tarehe 17 Machi, 2021. Kuondokewa na Jemedari wetu mahiri Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ni pigo kubwa si kwa Tanzania tu bali ni pigo kwa Afrika Mashariki, Bara la Afrika na Dunia nzima kwa ujumla.

5. ***Mheshimiwa Spika***, mchango mkubwa wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Taifa hili hautasahaulika kizazi hadi kizazi. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuenzi mchango wake hususan katika kuboresha Huduma za Afya ya Msingi, uboreshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari ikiwemo Elimumsingi Bila Malipo, miundombinu ya barabara za Vijijini na Mijini chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), usafiri na usafirishaji na uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi

katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**6. *Mheshimiwa Spika***, vilevile, naomba kutoa pole zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Hayati Benjamin William Mkapa; Maalim Seif Sharif Hamad*, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na *Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi*, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

**7. *Mheshimiwa Spika***, naomba nitoe pole nyingi kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu *Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla*, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara na *Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye*, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe. Taifa litakosa mchango wao katika kuisimamia Serikali kufanikisha maendeleo na ustawi



wa nchi yetu. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu na marafiki wa watanzania wenzangu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

**8. Mheshimiwa Spika,** nampongeza Mheshimiwa **Dkt. Philip Isidor Mpango** kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na Chama Cha Mapinduzi na baadae kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia shughuli za Serikali kwa mafanikio makubwa.

**9. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika, *Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansansu*, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuongoza Mhimili wa Bunge.

Tunawaahidi kuwapa ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

- 10. *Mheshimiwa Spika***, kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunitewa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Ninamshukuru pia kwa kuendelea kuwaamini *Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange*, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na *Mheshimiwa David Ernest Silinde*, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kuwa Naibu Mawaziri Ofisi ya Rais TAMISEMI. Tunamuahidi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na watanzania kuwa tutafanya kazi kwa bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu kwake na kwa nchi yetu katika kumsaidia kusimamia shughuli za utawala na maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan kwa kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kukusanya zaidi mapato ya ndani ili mapato hayo yaweze kutumika kutekeleza miradi

mbalimbali ya maendeleo na kuboresha huduma za jamii katika maeneo yao ikiwemo huduma za Afya ya Msingi, Elimu ya Msingi na Sekondari, Miundombinu ya barabara na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Aidha, tutaongeza jitihada za kusimamia matumizi ya fedha za umma katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- 11. *Mheshimiwa Spika***, kipekee, nampongeza *Mheshimiwa Humphrey Hezron Polepole (Mb)*, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, *Mheshimiwa Abdallah Jaffari Chaurembo (Mb)*, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, Kamati ilijadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2021/22 na kupitisha kwa kauli moja. Vilevile, Kamati imekuwa ikitoa ushauri

ambao umesaidia kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu na Taasisi nyingine zilizopo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika kuhudumia wananchi.

**12. *Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee naomba niipongeze Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia kikamilifu, kwa dhati na kwa umakini mkubwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambao umeiwezesha nchi kufikia Uchumi wa Kati na kutangazwa na Benki ya Dunia tarehe 01 Julai, 2020 kabla ya muda uliotarajiwa mwaka 2025.

**B. MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS – TAMISEMI (FUNGU 56), OFISI ZA WAKUU WA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAFUNGU 26) NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (FUNGU NA. 2)**

**13. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais  
- TAMISEMI inatekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuuji wa Madaraka (D by D), uratibu wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na maendeleo ya Miji na Vijiji;
- ii) Kuwezesha Tawala za Mikoa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;
- iii) Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;
- iv) Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma Mijini na Vijijini kama vile usafiri na usafirishaji, na usafi wa mazingira;
- v) Kuiwezesha Tume ya Utumishi wa Walimu kutekeleza majukumu yake;
- vi) Kusimamia utoaji wa huduma za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari;
- vii) Kusimamia utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

- viii) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi; na
- ix) Kusimamia utendaji wa Mashirika, Taasisi, Programu na Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

**14. Mheshimiwa Spika,** majukumu yanayotekelezwa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa ni kama ifuatavyo:

- i) Kuhakikisha kunakuwepo amani, usalama na utulivu katika Mikoa na Wilaya;
- ii) Kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iii) Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi;
- iv) Kufuatilia utekelezaji wa Mipango, Programu na Miradi mbalimbali zinazotekelezwa na Mikoa na

- Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo yao;
- v) Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
  - vi) Kusimamia na kuratibu utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
  - vii) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

**15. *Mheshimiwa Spika***, majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

- i) Kuhakikisha na kuwezesha utekelezaji wa Sheria na Ulinzi wa wananchi katika maeneo yao;
- ii) Kukuza ustawi wa jamii na uchumi

- wa wananchi wote katika maeneo yao;
- iii) Kukuza demokrasia na kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi yanayohusu ustawi na maendeleo yao;
  - iv) Kuhifadhi na kuendeleza mazingira ili kuweza kuwa na maendeleo endelevu ikiwa ni pamoja na kuwa na Mpango Mkakati wa Matumizi ya Ardhi;
  - v) Kutekeleza upelekaji wa madaraka ya kisiasa, fedha na utawala wa majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanayohusu kazi, uwezo, madaraka na huduma kwenye ngazi zote za Halmashauri;
  - vi) Kubuni na kuimarisha vyanzo vya mapato na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato;
  - vii) Kutoa huduma za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Watu Wazima;



- viii) Kutoa Huduma za Afya ya Msingi katika Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati na ngazi ya jamii;
- ix) Kuendeleza huduma za kilimo, uvuvi, ufugaji na ushirika;
- x) Kuendeleza shughuli za utamaduni, michezo na burudani;
- xi) Kusaidia na kuwezesha uratibu wa taasisi zisizo za kiserikali na taasisi za kijamii;
- xii) Kuendeleza biashara, kuchochea ukuaji wa uchumi, maendeleo ya viwanda na kuondoa umaskini;
- xiii) Kukuza ajira, ustawi wa jamii na vijana; na
- xiv) Kusimamia matumizi ya ardhi na maendeleo ya makazi.

**16. Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu yameainishwa

kwenye Kifungu cha 5 cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015 kama ifuatavyo:

- i) Kuendeleza na kusimamia utumishi wa walimu;
- ii) Kumshauri Waziri katika kusimamia na kuendeleza utumishi wa walimu;
- iii) Kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu;
- iv) Kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa walimu katika Halmashauri na kwenye shule;
- v) Kushughulikia masuala ya rufaa zinazotokana na maamuzi ya Mamlaka ya Nidhamu;
- vi) Kutunza daftari la kumbukumbu za walimu wote waliopo kwenye Utumishi wa Umma;
- vii) Kusimamia programu za mafunzo ya walimu kazini;
- viii) Kufanya utafiti na tathmini kuhusu masuala yanayohusu utumishi wa walimu na kumshauri Waziri;

- ix) Kutathmini hali ya walimu na kushauri Wizara yenye dhamana ya masuala ya walimu juu ya mafunzo, idadi na uhitaji wa walimu nchini;
- x) Kuandaa Kanuni na kusimamia maadili ya utendaji kazi wa walimu; na
- xi) Kuhakikisha kuwa waajiri na Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya wanatekeleza kazi zao kwa mujibu wa Sheria.

**C. TAARIFAYAUTEKELEZAJI WASHUGHULI ZA OFISI YA RAIS – TAMISEMI (FUNGU 56), MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAFUNGU 26) NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (FUNGU NA. 2) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

**17. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuzingatia dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na; kuratibu uimarishaji

wa utoaji Huduma za Afya ya Msingi kwa kujenga na kukarabati miundombinu na kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; kuratibu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu katika Shule za Msingi, Sekondari na nyumba za walimu kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuratibu usimamizi wa mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo.

- 18. *Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI pia imeendelea kuratibu usimamizi wa rasilimaliwatu na kuongeza ajira; kuratibu uimarishaji wamiundombinu ya barabara za Vijijini na Mijini; kuratibu uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Halmashauri; kuratibu usimamizi wa rasilimali fedha; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi; kuratibu usimamizi wa uwezeshaji wananchi kiuchumi; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kujenga miundombinu ya kiuchumi na

kijamii inayowezesha kufungua fursa za kiuchumi Mijini na Vijijini, kuendeleza na kusimamia utumishi wa walimu; pamoja na kuziwezesha Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) na Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) kwa Mwaka wa Fedha 2020/21**

- 19. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani jumla ya **Shilingi bilioni 860.95**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 45.77** ni Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, **Shilingi milioni 209.69** ni Maduhuli ya Mikoa na **Shilingi bilioni 814.96** ni Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hadi Februari

2021, jumla ya **Shilingi bilioni 495.25** zimekusanywa sawa na **asilimia 57.52** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**20. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa **Shilingi trilioni 7.01** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 3.87** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 851.14** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi trilioni 2.28** ni za Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 1.29** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 992.97** fedha za nje. Hadi Februari 2021, **Shilingi trilioni 3.90** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 55.66** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI  
(Fungu 56)**

- 21. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Taasisi zake (Fungu 56) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 703.44** kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 578.04** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 276.53** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 301.51** ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi bilioni 125.40** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 53.45** ni fedha za Mishahara na **Shilingi bilioni 71.95** ni fedha za Matumizi Mengineyo ikijumuisha **Shilingi bilioni 61. 28** za Kiinua Mgongo cha Madiwani.
- 22. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 384.54** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 54.66** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 103.79** ni fedha za Matumizi ya Kawaida

ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 32.21** ni fedha za Mishahara na **Shilingi bilioni 71.58** ni fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 280.75** ni fedha za Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 171.45** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 109.30** ni fedha za nje. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake imekusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani kiasi cha **Shilingi bilioni 22.77** sawa na **asilimia 50.00** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 45.77**, makusanyo hayo yametokana na mauzo ya vifaa chakavu, mauzo ya huduma, ada ya maegesho ya magari, ada za wanafunzi na tozo mbalimbali.

### **Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu - TSC (Fungu Na. 2)**

- 23. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 14.77**. Kati ya fedha



hizo, **Shilingi bilioni 14.27** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 8.17** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 6.10** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Tume iliidhinishiwa **Shilingi milioni 500.00** ambazo ni fedha za ndani.

- 24. Mheshimiwa Spika,** hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 7.64** zimepokelewa sawa na **asilimia 51.72** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 7.64** ni fedha za Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 4.13** ni fedha za Mishahara na **Shilingi bilioni 3.51** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

### **Bajeti za Mikoa Mafungu 26**

- 25. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Mikoa 26 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 221.88** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 135.88** ni kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 76.89** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 58.99** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi bilioni 85.99** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 57.72** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 28.27** ni fedha za nje. Hadi Februari 2021, **Shilingi bilioni 113.93** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 51.35** ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi bilioni 87.48** za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 26.45** ni fedha za Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 24.17** ni fedha za ndani.

- 26. *Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2021, Mikoa imekusanya Maduhuli ya **Shilingi milioni 74.45** sawa na **asilimia 36** ya lengo la kukusanya **Shilingi milioni 209.69**. Makusanyo ya Maduhuli yametokana na mauzo ya vifaa chakavu. Makusanyo ya Maduhuli ya Mikoa yamepungua kwa sababu ya kuanzishwa kwa utaratibu

wa kuomba zabuni kupitia mfumo wa kielektroniki wa TANEPS unaosimamiwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), hivyo mapato ya maombi ya zabuni yanawasilishwa PPRA.

## **Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa 26**

### **Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

- 27. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Halmashauri zilikasimiwa kukusanya **Shilingi bilioni 814.96** kutoka vyanzo vya Mapato ya Ndani. Hadi Februari, 2021 Halmashauri zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 473.94** sawa na **asilimia 58.16** ya bajeti iliyoidhinishwa. Makusanyo haya ni ongezeko la **Shilingi bilioni 5.95** ikilinganishwa na makusanyo ya **Shilingi bilioni 466.45** yaliyokusanywa hadi Februari 2020, kwa mwaka wa fedha 2019/20.

**28. Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa iliongezeka kutoka **Shilingi bilioni 765.48** katika mwaka wa fedha 2019/20 hadi **Shilingi bilioni 814.96** katika mwaka wa fedha 2020/21 sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 49.48 (Rejea Kiambatisho Na. 1).**

**Ruzuku ya Serikali Kuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kwenye Mikoja 26**

**29. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa kutumia **Shilingi trilioni 5.26.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 3.97** ni Matumizi ya Kawaida zikijumuisha Mishahara **Shilingi trilioni 3.74** na **Shilingi bilioni 232.21** ni Matumizi Mengineyo. Miradi ya Maendeleo ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.29** ambazo kati yake **Shilingi bilioni 629.10** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 663.18** ni fedha za nje. Hadi Februari

2021, jumla ya **Shilingi trilioni 2.92** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 55.51** ya bajeti, ambapo **Shilingi trilioni 2.50** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 422.78** ni fedha za Miradi ya Maendeleo kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 370.12** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 52.66** ni fedha za nje.

### **Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

- 30. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu zilipokea jumla ya **Shilingi trilioni 3.90** kati ya bajeti ya **Shilingi trilioni 7.01** sawa na **asilimia 55.63**. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi trilioni 3.03** ambapo Mishahara ni **Shilingi trilioni 2.42** na **Shilingi bilioni 615.91** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi bilioni 870.77** ni fedha za Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 706.54** ni fedha za ndani na kiasi

cha **Shilingi bilioni 164.23** ni fedha za nje  
(*Rejea Kiambatisho Na. 2*).

**Utekelezaji wa Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi Februari, 2021 kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa**

- 31. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21 Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu imetekeleza mpango kama ifuatavyo:

### **HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI**

- 32. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika uboreshaji wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uboreshaji huu utawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii na kuchochea maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Ofisi ya

Rais – TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa afua hizi katika Halmashauri zote nchini.

### **Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya**

- 33. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Halmashauri **99**, Vituo vya Afya **487** na ujenzi wa Zahanati **1,198**. Aidha, kwa kutumia Mapato ya Ndani, Halmashauri za Jiji la Arusha, Mwanza na Manispaa ya Kinondoni zimeanza ujenzi wa Hospitali na kufanya Hospitali za Halmashauri zinazojengwa kuongeza na kufikia **102**.
- 34. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 119.75** kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba, ambapo **Shilingi bilioni 32.50** ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Wodi **201** katika

Hospitali **67**, ununuzi wa vifaa tiba kwa Hospitali **67 Shilingi bilioni 32.50**, ujenzi wa Hospitali Mpya **27 Shilingi bilioni 27.00** na **Shilingi bilioni 27.75** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya Zahanati **555**, ikiwa ni wastani wa maboma **3** kwa kila Halmashauri. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 58.99** sawa na **asilimia 49.26** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo (*Rejea Kiambatisho Na. 3*).

### **Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi**

**35. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutoa Huduma za Afya ngazi ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Februari 2021, vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi **5,838** vimetoa huduma kwa wagonjwa wapatao **23,209,724** ambapo wanawake ni **13,943,539** na wanaume ni **9,266,185**. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa, wagonjwa **15,619,410** sawa na **asilimia 67** walipatiwa huduma za Wagonjwa wa



Nje (OPD) na wagonjwa **7,590,314** sawa na **asilimia 33** walipatiwa huduma za Wagonjwa wa Ndani (IPD).

### **Usafi wa Mazingira**

**36. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kusimamia shughuli za usafi wa mazingira katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambapo vituo vya afya ya msingi **860** vinaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji safi na vyoo bora katika Halmashauri **86** nchini. Hadi Februari 2021, zimetolewa **Shilingi bilioni 18.9** kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo.

### **Udhibiti wa Magonjwa ya Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi**

**37. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais -TAMISEMI

imesimamia ugawaji wa vyandarua **12,797,038** vyenye viuatilifu vya muda mrefu kupitia programu za ugawaji wa vyandarua ngazi ya jamii, shule na vituo vya kutolea huduma za afya. Vyandarua hivi viligawiwa kwenye Mikoa **10** yenye maambukizi ya wastani ya Rukwa, Songwe, Njombe, Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Manyara, Kilimanjaro na Tanga. Aidha, vyandarua vilitolewa kwenye Mikoa **14** yenye maambukizi makubwa ya Lindi, Ruvuma, Mtwara, Morogoro, Pwani, Katavi, Tabora, Kigoma, Kagera, Geita, Mwanza, Simiyu, Mara na Shinyanga. Vilevile, Mikoa yote imepata vyandarua kupitia kliniki za mama, baba na mtoto.

- 38. *Mheshimiwa Spika***, utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na UKIMWI umeboreshwa kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyoko katika Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu UKIMWI na Virusi vya UKIMWI. Elimu inayotolewa

katika vituo hivi imetoa mchango mkubwa katika kupunguza unyanyapaa kwenye jamii na kuongeza idadi ya wagonjwa wanaojitokeza kupima afya zao ikiwa ni pamoja na kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

### **Huduma Za Lishe**

- 39. *Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya lishe duni katika jamii, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha Kamati za Lishe za Mikoja **26** na Halmashauri **184** kote nchini zenye jukumu la kujadili na kutatua changamoto za lishe katika maeneo yao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo. Katika kufanikisha jukumu hili, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusaini mikataba ya utendaji na usimamizi wa masuala ya lishe katika ngazi zote na kufanyiwa tathmini. Mikataba hii imeongeza uwajibikaji katika usimamizi wa afua za lishe.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha tathmini ya shughuli za lishe, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imefanya maboresho ya Mfumo Jumuishi wa Tathmini na Ufuatiliaji (*Integrated Monitoring and Evaluation System – IMES*) kwa ajili ya kukusanya taarifa za kiuchumi na kijamii zikiwemo taarifa za lishe katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazojumuisha taarifa ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya. Taarifa hizi zitatumika kuboresha mikakati ya nchi dhidi ya utapiamlo na itasaidia kuelekeza rasilimali fedha kulingana na ukubwa wa tatizo kwa mujibu wa takwimu.

### **Huduma za Watu Wenye Ulemavu**

**41. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kuratibu huduma za Watu Wenye Ulemavu katika Mamlaka za Serikaliza Mitaa ambapo hadi Februari 2021, jumla ya Watu Wenye Ulemavu wapatao **124,900** kati yao wanawake **59,059** na wanaume **65,841** wametambuliwa sawa na **asilimia 83** ya lengo. Vilevile, kaya

**196,372** zimetambuliwa kupitia mfuko wa TASAF na zinasubiri kuhakikiwa ili ziweze kupatiwa ruzuku. Aidha, Kamati za Watu Wenye Ulemavu zimeundwa na kuratibiwa kwenye Mikoa **26** sawa na **asilimia 100.00** na Halmashauri **184** sawa na **asilimia 99.46**. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imetumia kiasi cha **Shilingi bilioni 1.30** kwa ajili ya kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu wapatao **15,596** kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii, vifaa saidizi kama vile viti mwendo, baiskeli na pikipiki za magurudumu matatu, fimbo nyeupe na miwani.

### **Huduma ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto**

- 42. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mtoto na Mwanamke zimeundwa katika

Mikoa **26**, Halmashauri **184**, Kata **2,840** kati ya **3,956** na Vijiji **7,970** kati ya Vijiji **12,319**. Hatua za kuunda Kamati kwenye Kata na Vijiji vilivyobaki zinaendelea. Aidha, kampeni za kutokomeza mimba na ndoa za utotoni zinaendelea kutekelezwa katika Halmashauri zote. Vilevile, Wataalam wa Ustawi wa Jamii **684** kati ya **740** wamepatiwa mafunzo kuhusu namna ya kutoa huduma ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika maeneo yao.

- 43. *Mheshimiwa Spika***, mashauri ya watoto wanaokinza na Sheria na waliofanyiwa ukatili yanaendelea kupokelewa na kushughulikiwa ambapo hadi Februari 2021, jumla ya mashauri **27,470** ya watoto waliofanyiwa ukatili na watoto **11,837** wanaokinza na sheria yameshughulikiwa. Aidha, jumla ya watoto **39,307** waliofanyiwa vitendo vya ukatili na watoto wanaokinza na sheria walipatiwa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii na kuunganishwa na familia zao.

**44. Mheshimiwa Spika,** huduma za watoto walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani zimeendelea kuwa kipaumbele kwa kuwatambua na kuwaunganisha na huduma mbalimbali zikiwemo huduma za Afya, Elimu, Bima ya Afya na VVU/UKIMWI. Hadi Februari 2021, jumla ya watoto **472,790** wanaoishi katika mazingira hatarishi wametambuliwa ambao ni sawa na **asilimia 90.00** ya lengo.

#### **Huduma za Wazee**

**45. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuwatambua na kuwapatia wazee wasiojiweza vitambulisho vya matibabu bila malipo kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2007. Hadi Februari 2021, jumla ya Wazee **366,252** wametambuliwa katika Mikoa yote wakiwemo wanawake **195,771** na wanaume **170,481** ambapo kati ya hao waliopatiwa vitambulisho vya wazee baada

ya kukidhi vigezo vya Sera hiyo ya Afya ni **214,141**.

**46. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha utendaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee ambapo hadi Februari 2021 Mabaraza **3,456** ya Ushauri ya Wazee yameundwa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya wazee katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jumla ya wazee **128,820** wamepatiwa huduma za matibabu ya afya bila malipo na jumla ya **Shilingi bilioni 3.2** zimetumika kugharamia matibabu ya wazee kwa ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo.

### **Matibabu ya Afya kwa Msamaha**

**47. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais -TAMISEM imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa makundi maalum ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 29.3** zimetumika kugharamia matibabu bila malipo kwa wagonjwa **11,423,444** kutoka makundi



maalum ambayo yanayohusisha wazee wenye umri wa miaka zaidi ya 60 na wasio na uwezo, wafungwa, watoto chini ya miaka mitano, wajawazito, wasiojiweza kiuchumi, watu wenye magonjwa sugu na Watu Wenye Ulemavu.

### **Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF)**

**48. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 katika **Ibara ya 186** inaelekeza kuimarisha utaratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) ili iwafikie wananchi walio wengi na hasa wanyonge. Aidha, Ilani inaelekeza kutekeleza mikakati ya kuhamasisha wananchi wajiunge na huduma za Bima ya Afya.

**49. Mheshimiwa Spika,** hadi Februari 2021 Mikoa yote nchini imefanikiwa kutekeleza Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) ambapo uandikishaji unaendelea katika Mitaa na Vijiji vyote nchini. Maendeleo ya utekelezaji huu yamewezesha kufikiwa kwa mafanikio yafuatayo:

- i) Jumla ya wanachama **3,300,000** wamejiunga na Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) sawa na asilimia 6 ya Watanzania wote;
- ii) Jumla ya **Shilingi bilioni 17.1** zimekusanywa kutokana na michango ya wanachama;
- iii) Jumla ya **Shilingi bilioni 2.3** zimelipwa na Serikali ikiwa ni fedha za tele kwa tele na kufanya kiasi cha makusanyo yote kuwa **Shilingi bilioni 19.4**;

Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Februari, 2021 wanachama **milioni 1** wamenufaika na Bima hii kwa kuweza kufikia Huduma za Afya kwa kupata matibabu katika vituo vya kutolea

Huduma za Afya ya Msingi, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 6.7** zimelipwa kwenye vituo hivyo.

## **Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari**

**50. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Elimu ya Msingi na Sekondari kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutekeleza yafuatayo:

- i) Kusimamia utoaji wa huduma kwa wanafunzi **14,990,844** ambapo wanafunzi **1,198,564** ni wa Shule za Awali, **11,035,064** Shule za Msingi (Darasa la Kwanza hadi Darasa la Saba) na Wanafunzi **2,757,216** ni wa Shule za Sekondari (Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Nne). Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inasimamia jumla ya walimu **261,253** ambapo

- walimu **175,887** ni wa Shule za Msingi na walimu **85,366** ni wa Shule za Sekondari.
- ii) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari. Miundombinu inayoendelea kujengwa ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi ni pamoja na vyumba vya madarasa **5,224**, matundu ya vyoo **15,616**, nyumba za walimu **38**, mabweni **223**, mabwalo **40**, majengo ya utawala **21** na vyumba vya maabara za sayansi **902**;
  - iii) Kubainisha watoto wenye mahitaji maalum katika Halmashauri 184 ambapo jumla ya wanafunzi 28,698 (wavulana **16,461** na wasichana **12,237**) walibainishwa na kupangiwa shule kulingana na mahitaji yao;
  - iv) Jumla ya vituo **510** vya walimu vimeainishwa kwa ajili ya kuviboresha ili kutoa mafunzo ya walimu kazini karibu na maeneo yao;
  - v) Kuratibu mitihani ya kitaifa ya

- Darasa la Saba, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita na upimaji Darasa la Nne na Kidato cha Pili;
- vi) Kuratibu ajira na kupanga vituo vya kazi kwa walimu na Mafundi Sanifu wa maabara **8,000** wa Shule za Msingi na Sekondari; na
  - vii) Kuwapangia shule wanafunzi wote **833,672** waliofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2020.

**51. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha na kuboresha kiwango cha elimu kuanzia ngazi ya Awali, Msingi na Sekondari kwa kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo, uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari kama ifuatavyo:

## **Elimu ya Msingi**

### **Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Msingi kwa mwaka 2021**

- 52. *Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2021, uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali ulifikia wanafunzi **1,057,919** sawa na **asilimia 83.14** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,272,513** ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo wanafunzi **1,278,016** sawa na asilimia **92.48** waliandikishwa kati ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,382,761** (*Rejea Kiambatisho Na. 4*).
- 53. *Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2021, jumla ya wanafunzi wa Darasa la Kwanza **1,400,145** sawa na **asilimia 92.32** ya lengo la uandikishaji wa wanafunzi **1,516,598** ulifikiwa ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo wanafunzi **1,526,474** waliandikishwa sawa na **asilimia 96** ya lengo la uandikishaji wa wanafunzi **1,597,612**. Kuendelea kupungua kwa uandikishaji unatokana na mafanikio

ya Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo uliowezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kwa sababu ya kuondolewa kwa ada na michango mbalimbali (***Rejea Kiambatisho Na. 5***).

### **Uboreshaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi**

- 54. *Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2021 jumla ya vyumba vya madarasa **3,049** vya Shule za Msingi vimejengwa na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **125,719** vilivyokuwepo Februari, 2020 hadi vyumba vya madarasa **128,768**. Jumla ya matunduyavyoo **14,581** yamejengwa katika Shule za Msingi na kuongeza matundu ya vyoo kutoka **205,663** vilivyokuwepo Februari, 2020 hadi kufikia matundu ya vyoo **220,244** mwezi Februari, 2021. Ongezeko la miundombinu hii imesaidia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Vilevile, jumla ya nyumba za walimu **20** zimejengwa katika Shule za Msingi katika kipindi hicho.

**55. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali iliidhinisha jumla ya **Shilingi bilioni 26.10** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa **2,088** katika Halmashauri **184**. Hadi Februari 2021, kiasi cha **Shilingi bilioni 18.22** kimetolewa sawa na **asilimia 69.81** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **1,360** ya vyumba vya madarasa ya Shule za Msingi. **(Rejea Kiambatisho Na.6).**

**56. Mheshimiwa Spika,** kazi za ujenzi wa vyumba vya madarasa imekwenda sambamba na utengenezaji wa madawati. Hadi Februari 2021, idadi ya madawati imefikia **3,113,741** ikilinganishwa na madawati **3,052,541** yaliyokuwepo mwezi Februari 2020, ikiwa ni ongezeko la madawati **61,200**.

### **Mtihani wa Upimaji wa Darasa la Nne na Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba**

**57. Mheshimiwa Spika,** katika matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka



2019, jumla ya wanafunzi **1,531,120** kati ya wanafunzi **1,665,863** sawa na **asilimia 91.9** walikidhi sifa za kuendelea Darasa la Tano, ikilinganishwa na wanafunzi **1,551,599** kati ya wanafunzi **1,704,286** sawa na **asilimia 91.04** ya waliofanya mtihani huo mwaka 2020.

- 58. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020, ufaulu wa mtihani wa kuhitimu Darasa la Saba umeongezeka kutoka **asilimia 81.50** mwaka 2019 hadi **asilimia 83.15** mwaka 2020. Kwa mwaka 2020, jumla ya wanafunzi **833,872** walifaulu sawa na **asilimia 83.15** kati ya wanafunzi **1,008,307** waliofanya mtihani, ikilinganishwa na wanafunzi **759,737** sawa na **asilimia 81.50** waliofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi kati ya wanafunzi **933,369** waliofanya mtihani mwaka 2019.

## **Elimu ya Sekondari**

### **Usajili wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza**

**59. Mheshimiwa Spika,** idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika Shule za Sekondari nchini imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi. Kwa mwaka 2021, jumla ya wanafunzi **833,872** walichaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi **759,737** waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2019 (*Rejea Kiambatisho Na. 7*).

### **Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Shule za Sekondari**

**60. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuboresha miundombinu ya Shule za Sekondari ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari wanapata fursa ya kuendelea na masomo. Hadi Februari 2021, jumla ya madarasa mapya **936**, matundu ya vyoo **1,035**, mabweni **223**, mabwalo **40**, maktaba **8**, maabara za sayansi **18**, majengo

ya utawala **21** na nyumba za walimu **18** zimejengwa. Vilevile, ukarabati wa Shule Kongwe **13** za Sekondari ambazo ni Shule za Sekondari za Iringa Wasichana, Tumaini Wasichana, Mwanza, Masasi Wasichana, Ashira Wasichana, Kibasila, Tarime, Shinyanga, Rungwe, Lindi, Moshi, Arusha Wasichana na Tunduru ambazo ziko katika hatua ya ukamilishaji kwa gharama ya **Shilingi bilioni 19.88**. Idadi hii inafikisha Shule Kongwe **86** zilizokarabatiwa kati ya Shule **89** sawa na **asilimia 96.63** ya lengo.

### **Ukamilishaji wa Vyumba vya Maabara za Masomo ya Sayansi**

- 61. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kutoa kipaumbele katika ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo kwenye Shule za Sekondari. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imefuta mitihani ya sayansi mbadala wa vitendo (Alternative to Practicals) iliyodumu tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990 baada ya miaka zaidi ya 25. Wanafunzi wote wa

Kidato cha Nne 2020 wamefanya mitihani ya Sayansi kwa vitendo. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 26.51** zimetolewa kati ya **Shilingi bilioni 42.33** sawa na **asilimia 62.63** zilizoidhinishwa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara **1,411** za sayansi *(Rejea Kiambatisho Na. 6)*

**62. Mheshimiwa Spika,** sambamba na uboreshaji wa miundombinu mingine ya Shule za Sekondari, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kutoa kipaumbele katika ujenzi wa matundu ya vyoo, mabweni na nyumba za walimu. Hadi Februari 2021, jumla ya matundu ya vyoo **1,035** yamejengwa kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 1.14**, mabweni **223** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **80** kila moja kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 17.84** na nyumba za walimu **18** kwa kiasi cha **Shilingi milioni 900**.

**63. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha Shule za Sekondari za Ufundi kwa kuajiri na kuwapangia vituo walimu wa masomo ya

ufundi wa fani mbalimbali katika Shule zote tisa (9) za Sekondari za Ufundi ambazo ni Moshi Ufundi, Musoma Ufundi, Iyunga Ufundi, Ifunda Ufundi, Mtwara Ufundi, Tanga Ufundi, Bwiru Ufundi, Mwadui Ufundi na Chato Ufundi. Shule hizo zimekarabatiwa na kupewa kipaumbele cha kupangiwa walimu. Aidha, Shule hizo zimetengewa **Shilingi milioni 500.00** kwa kila shule kwa ajili ya kununua vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia ili kuwawezesha wahitimu kuwa na uwezo wa kujiajiri au kuendelea na masomo ya juu katika vyuo vya ndani na nje ya nchi.

### **Mtihani wa Upimaji wa Kidato cha Pili na Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne na Sita**

- 64. *Mheshimiwa Spika***, matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili katika mwaka 2020 yameonesha ongezeko la ufaulu kati ya mwaka 2019 na 2020 kwa **asilimia 1.57** ambapo mwaka 2019 jumla ya wanafunzi

**514,251** kati ya wanafunzi **571,137** waliofanya mtihani sawa na **asilimia 90.04** walifaulu mtihani huo na kuendelea na Kidato cha Tatu, ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo jumla ya wanafunzi **601,948** waliofanya mtihani huo na wanafunzi **550,979** walifaulu sawa na **asilimia 91.61**.

**65. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Kidato cha Nne, ufaulu umeongezeka kutoka **asilimia 80.65** mwaka 2019 hadi **asilimia 85.84** mwaka 2020. Mwaka 2019 wanafunzi **340,914** walifaulu kati ya wanafunzi **422,722** waliofanya mtihani na mwaka 2020 wanafunzi **373,958** walifaulu kati ya wanafunzi **437,698** waliofanya mtihani sawa na ongezeko la **asilimia 5.19**.

**66. Mheshimiwa Spika**, ufaulu wa Kidato cha Sita kwa mwaka 2020 ulikuwa ni **asilimia 99.51** ambapo watahiniwa **73,537** kati ya watahiniwa **73,901** waliofanya mtihani walifaulu ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo watahiniwa **78,666** kati ya **79,770** ya waliofanya mtihani walifaulu sawa na **asilimia 98.61** ya watahiniwa. Ufaulu wa

Kidato cha Sita umeendelea kuwa bora zaidi kila mwaka.

**Utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo.**

- 67. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo ulioanza Desemba, 2015. Kuanzia Julai, 2020 hadi Februari 2021, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 166.44** kwa ajili ya kutekeleza Mpango huo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi bilioni 80.51** na **Shilingi bilioni 85.93** zilitumika katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari mtawalia (**Rejea Kiambatisho Na.8 kwa Shule za Msingi na Rejea Kiambatisho Na.9 kwa Shule za Sekondari**). Aidha, kiasi cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya Elimumsingi Bila Malipo kuanzia Desemba 2015 hadi Februari 2021, ni **Shilingi trilioni 1.26**
- 68. Mheshimiwa Spika,** hadi Februari 2021, maeneo yaliyopatiwa fedha za ruzuku za

Elimu Msingi Bila Malipo ni: uendeshaji wa shule **Shilingi bilioni 54.59**, chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi na wanafunzi wa bweni wa Shule za Sekondari **Shilingi bilioni 49.49**.

- 69. Mheshimiwa Spika**, maeneo mengine yaliyopatiwa fedha ni fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na bweni wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne **Shilingi bilioni 20.53**, posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata **Shilingi bilioni 41.83**. Posho ya madaraka inayotolewa kila mwezi kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata imeongeza ufanisi wa utendaji kazi wa viongozi hao.

### **Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

- 70. Mheshimiwa Spika**, uandikishaji wa wanafunzi wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Matokeo ya uandikishaji kwa mwaka 2020



yanaonesha kupungua ambapo wanafunzi **56,560** wakiwemo wavulana **31,728** na wasichana **24,832** waliandikishwa. Idadi hiyo imepungua kwa **asilimia 15.6** ikilinganishwa na wanafunzi **66,978** wakiwemo **wavulana 38,567 na wasichana 28,411** walioandikishwa mwaka 2019.

**71. Mheshimiwa Spika,** kupungua kwa uandikishaji kunatokana na mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Elimummsingi Bila Malipo ambapo kuanzia mwaka 2015 hadi Februari 2021 mpango umewezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kutokana na kuondolewa kwa ada na michango mbalimbali ambayo ilikuwa ni miongoni mwa vikwazo vilivyopunguza kiwango cha uandikishaji. Hii inaashiria kwamba wanafunzi waliokuwa wanakosa nafasi ya elimu katika mfumo rasmi sasa wanapata fursa hiyo. Aidha, uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule unafanyika kwa wakati.

**72. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na utekelezaji wa Elimu ya Watu Wazima kupitia Programu ya Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo Rasmi wa Shule (*Intergrated Programme for Out of School Adolescent - IPOSA*). Mpango huu unalenga kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na stadi za maisha vijana wenye umri wa miaka **14** hadi **19** katika maeneo ya ufugaji nyuki, samaki, kuku, useremala, uashi, utengenezaji batiki, usindikaji vyakula, utengenezaji mishumaa, sabuni, utengenezaji mafuta ya mwili pamoja na ushonaji. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, jumla ya walimu **258** walipatiwa mafunzo haya na jumla ya wanafunzi **9,939** wamesajiliwa na kuanza kusoma katika vituo **72** kwenye Mikoa nane (8) ya Kigoma, Tabora, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Dar es Salaam na Dodoma.

### **Elimu Maalum**

**73. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais –

TAMISEMI inasimamia Shule Maalum **37** za bweni, Vitengo Maalum **709** vinavyoshughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule za Msingi na Shule Jumuishi **2,952** zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi. Kwa upande wa Sekondari, kuna Shule Maalum moja (**1**) ya Patandi na vitengo maalum **81**. Hadi Februari 2021, uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum umeongezeka hadi kufikia wanafunzi **66,083** ambapo Shule za Msingi zina wanafunzi **55,758** na Shule za Sekondari zina wanafunzi **10,325** ikilinganishwa na wanafunzi **55,185** wenye mahitaji maalum waliokuwepo mwaka 2020. Idadi hii inahusisha wanafunzi wenye ulemavu wa masikio, macho, uoni hafifu, usonji, viungo na akili.

- 74. *Mheshimiwa Spika***, mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **1,461** wenye mahitaji maalum sawa na **asilimia 77.22** walifaulu mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi na kuchaguliwa kujiunga na Shule za

Sekondari kati ya wanafunzi **1,892** waliofanya mtihani. Katika mwaka 2020, jumla ya wanafunzi **2,487** sawa na **asilimia 98.1** walifaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi. Matokeo haya yanaonesha ongezeko la ufaulu kwa **asilimia 20.88**.

**75. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeajiri walimu **766** waliosomea taaluma ya Elimu Maalum ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata elimu sawa na wanafunzi wengine. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza vifaa visaidizi **51,339** vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 3**.

### **Michezo Shuleni**

**76. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeendelea kuhimiza na kusimamia maendeleo ya michezo katika Shule za Msingi na Sekondari. Wanafunzi na walimu waliendelea kuhamasishwa kushiriki katika mazoezi ya michezo kama

njia mojawapo ya kujikinga na maradhi. Ili kuendeleza michezo, jumla ya wanafunzi **1,669** katika Shule **79** za michezo walifanya mtihani wa somo la Elimu kwa Michezo katika mitihani ya Kidato cha Nne iliyofanyika mwezi Novemba, 2020.

- 77. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kuimarisha michezo kwa kuanzisha tahasusi ya Elimu ya Michezo kwa Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari na kutoa mafunzo kwa walimu **400** wa michezo ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo katika Shule za Msingi na Sekondari.

### **Ajira Zilizotolewa Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

- 78. *Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua mahitaji ya walimu katika Shule za Msingi na Sekondari, Serikali imeendelea kutoa ajira za walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kukabiliana na upungufu uliopo. Hadi Februari 2021, walimu **4,700** wa Shule za Msingi na walimu **3,300** wa

Shule za Sekondari waliajiriwa na Serikali inakamilisha taratibu za ajira ya walimu wengine **6,734**.

**Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Utawala na Nyumba za Viongozi Katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**79. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuratibu usimamizi wa ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, nyumba za makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na nyumba za Maafisa Waandamizi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea na ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Songwe, Njombe, Geita na Mbeya. Aidha, ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Mikoa ya Katavi na Njombe unaendelea, ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe umekamilika na zinatumiwa, nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe zipo katika hatua ya ukamilishaji. Vilevile,

Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba kumi **(10)** za Maafisa Waandamizi katika Mkoa wa Shinyanga, ambapo nyumba moja imekamilika.

**80. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea na ujenzi wa majengo ya utawala ya Wakuu wa Wilaya ambapo majengo matano **(5)** ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Mkalama, Ikungi, Mbogwe, Nyang’hwale na Buhigwe pamoja na Ofisi za Maafisa Tarafa **38** ujenzi unaendelea katika Mikoa ya Tanga Ofisi ishirini na moja **(21)**, Mwanza Ofisi kumi na nne **(14)** na Kigoma Ofisi tatu **(3)**. Aidha, nyumba nne **(4)** za Wakuu wa Wilaya za Bagamoyo, Kisarawe, Mkuranga na Bunda zimefanyiwa ukarabati. Hadi Februari 2021, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya utawala na nyumba za Viongozi ni **Shilingi bilioni 11.77** kati ya **Shilingi bilioni 50.43** zilizoidhinishwa.

**81. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea

kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kutoa huduma kwa wananchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kujenga majengo ya utawala na nyumba za makazi ya Wakurugenzi na Wakuu wa Idara. Jumla ya majengo ya utawala **100** yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kati ya majengo hayo, majengo **31** yapo katika hatua ya ukamilishaji, majengo **36** ujenzi unaendelea na **33** yamepangwa kuanza ujenzi yakiwemo majengo ya Halmashauri **30** zilizohamisha Makao Makuu kwenda katika maeneo yake ya utawala. Katika mwaka wa fedha 2020/21, **Shilingi bilioni 80.42** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa majengo ya utawala katika Halmashauri **100** ambapo hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 44.19** zimetolewa sawa na **asilimia 54.94. (Rejea Kiambatisho Na. 10)**

**82. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kuishi kwa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya



**Shilingi bilioni 1.35** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara katika Halmashauri za Wilaya za Wanging'ombe, Arusha, Karatu, Longido, Meru, Monduli, Ngorongoro, Pangani na Halmashauri ya Mji wa Mafinga na Halmashauri ya Jiji la Arusha. Hadi Februari 2021, **Shilingi milioni 593.17** sawa na **asilimia 43.94** zimetolewa.

### **Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

- 83. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kusimamia utoaji wa Mikopo ya Uwezeshaji kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa mujibu wa Kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019.
- 84. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi bilioni**

**64.5** zilitengwa na Halmashauri zote nchini kwa ajili ya mikopo kwa Vikundi **18,244** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 25.8** zilitengwa kwa ajili ya Vikundi **8,223** vya Wanawake, **Shilingi bilioni 25.8** kwa ajili ya Vikundi **6,966** vya Vijana na **Shilingi bilioni 12.9** kwa ajili ya Vikundi **3,055** vya Watu Wenye Ulemavu.

**85. Mheshimiwa Spika**, utoaji wa mikopo ya **asilimia 10** kutokana na Mapato ya Ndani ya Halmashauri umeendelea kuimarika ambapo hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 26.81** sawa na **asilimia 41.61** ya lengo la **Shilingi bilioni 64.46** zilikuwa zimetolewa kwa Vikundi **5,973** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imehuisha Kanuni za Utekelezaji wa uwezeshaji wa asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa ajili ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kupunguza idadi ya wanachama wanaoweza kuunda kikundi

kutoka wanachama 10 hadi watano (5) ambapo kwa upande wa Watu Wenye Ulemavu kikundi kinaweza kuundwa na watu wasiopungua wawili (2) kutoka idadi ya watu watano (5); kutumia sehemu ya fedha za marejesho kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini ya vikundi; mafunzo ya ujasiriamali; uongozi; usimamizi wa fedha na utoaji wa taarifa.

**86. Mheshimiwa Spika,** Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo nchini wameendelea kutambua umuhimu wa kutumia vitambulisho vya wajasiriamali ili biashara zao zitambulike na kuondokana na usumbufu waliokuwa wanaupata. Kuanzia tarehe 1 Machi, 2020 hadi Februari 2021, wafanyabiashara **716,776** wamepatiwa vitambulisho ambavyo vimewezesha kukusanywa kwa jumla ya **Shilingi bilioni 14.33** katika Mikoayoote **26** ya Tanzania Bara. Aidha, tangu kuanza kwa zoezi la utoaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo nchini jumla ya vitambulisho **2,335,711** vimegawiwa

ambavyo vimewezesha kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 46.71**. Lengo ni kuendelea kuwatambua wafanyabiashara wadogo na kuwawekea mazingira rafiki ya ufanyaji biashara. Katika mwaka 2020/21, Serikali imefanya maboresho ya vitambulisho vya Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo Nchini kwa kuweka picha na jina la mjasiriamali ili kuongeza udhibiti na kufungua fursa kwa wajasiriamali kuweza kutumia vitambulisho hivyo kupata huduma za kibenki na bima ya afya.

### **Miradi ya Kimkakati**

- 87. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali ilitenga jumla ya **Shilingi bilioni 50** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Miradi **38** ya Kimkakati yenye thamani ya **Shilingi bilioni 273.06**. Miradi hii inatekelezwa katika awamu mbili ambapo katika awamu ya kwanza jumla ya Halmashauri **17** zenye Miradi **22** zilifuzu vigezo na kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 131.77** na awamu ya pili jumla ya

Halmashauri **13** zenye miradi **16** zilifuzu vigezo na kutengewa jumla ya **Shilingi bilioni 141.59**. Hadi Februari, 2021 kiasi cha **Shilingi bilioni 44.15** kimetolewa sawa na asilimia **88.3** ya lengo la **Shilingi bilioni 50**.

**88. *Mheshimiwa Spika***, hadi Februari, 2021 utekelezaji wa miradi ya Kimkakati umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Miradi sita (6) katika Halmashauri za Wilaya za Kakonko (Soko la Muhange), Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu (Kituo cha Mabasi) na Ruangwa (Ghala la Mazao), Manispaa ya Morogoro (Soko la Chifu Kingalu), Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Soko la Kisutu) na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo (Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli kilichopo Mbezi Luis), utekelezaji wa miradi hii umekamilika na kuanza kutoa huduma. Aidha, miradi thelathini na mbili (**32**) inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

## **Huduma za Kiuchumi na Uzalishaji**

### **Maeneo ya Uwekezaji**

- 89. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuweka kipaumbele katika kutenga maeneo ya uwekezaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, jumla ya hekta **2,359,379.33** zimetengwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uwekezaji zikiwemo hekta **117,379.62** sawa na **asilimia 4.97** kwa ajili ya viwanda vikubwa, vidogo na vya kati. Aidha, hekta **1,216,242.17** sawa na **asilimia 51.54** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya madini, biashara, kilimo na skimu za umwagiliaji. Vilevile, hekta **1,025,756.64** sawa na **asilimia 43** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya malisho ya mifugo. Hivyo, wadau mbalimbali wanahamasishwa kutumia fursa hiyo ya uwekezaji.

## **Sekta ya Kilimo na Viwanda**

- 90. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wadau mbalimbali katika sekta ya Kilimo imeendelea kuratibu shughuli za kilimo hususan eneo la huduma za ugani. Hadi Februari 2021, jumla ya mashamba darasa **214** yameandaliwa ili kutoa elimu kwa vitendo kwa wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- 91. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi ya Alliance for Green Revolution in Africa (AGRA) imewajengea uwezo Wataalam wa Kilimo kuhusu kuandaa Mipango bora ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (DADPs) katika Mikoa **12** na Halmashauri za Wilaya **30** nchini. Mikoa hiyo ni Kagera (Muleba, Misenyi, Biharamulo); Kigoma (Kasulu, Kibondo, Kakonko); Katavi (Tanganyika, Mpimbwe, Nsimbo); Rukwa (Kalambo, Nkasi, Sumbawanga); Ruvuma (Songea, Madaba, Mbinga); Njombe (Wanging'ombe,

Ludewa); Iringa (Mufindi, Kilolo); Manyara (Babati, Hanang', Kiteto); Arusha (Meru, Karatu, Arusha); Kilimanjaro (Hai, Siha, Rombo); Simiyu (Maswa) na Tanga (Kilindi). Aidha, jumla ya wataalam **588** kutoka kwenye Mikoa hiyo na Halmashauri wamejengewa uwezo.

**92. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuboresha mifumo ya kuhifadhi mazao ya nafaka ili kuimarisha usalama wa chakula. Hadi Februari 2021, maghala sita (**6**) ya kuhifadhia mazao yenye uwezo wa kuhifadhi tani zaidi ya **18,000** yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Muleba, Rufiji na Momba kwa gharama ya **Shilingi milioni 278.06**. Vilevile, masoko matano (**5**) ya mazao ya kilimo yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Geita, Ulanga, Muheza na Halmashauri ya Mji wa Kibaha kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.35**. Masoko haya yatawezesha wakulima kuwa na sehemu ya uhakika na salama ya kuuzia mazao yao. Aidha, kwa upande wa uendelezaji viwanda hadi



Februari 2021, jumla ya viwanda **1,490** vimejengwa vikiwemo viwanda vikubwa **45**, vya kati **153**, vidogo **593** na vidogo sana **699**. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda ili kuzalisha ajira na kupunguza umasikini.

### **Sekta ya Mifugo**

**93. *Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na magonjwa ya mifugo yanayotokana na kupe na aina nyingine ya maambukizi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeratibu ujenzi na ukarabati wa majosho **277** kwa gharama ya **Shilingi milioni 357.28**. Majosho haya yapo katika Mikoa **15** ya Kigoma, Katavi, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Ruvuma, Morogoro, Mwanza, Rukwa, Tabora, Shinyanga, Tanga, Simiyu na Songwe. Aidha, zaidi ya mifugo **milioni 12** imeogeshwa ambapo gharama za madawa zilichangiwa na wananchi ambao ni wafugaji.

## **Maliasili na Mazingira**

- 94. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia Sera na Mikakati mbalimbali ya kuhifadhi mazingira kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali. Hadi Februari 2021, Ofisi imeratibu uandaaji wa vitalu ambapo jumla ya miche ya miti ya matunda, mbao na ya kuhifadhi mazingira **milioni 170** imepandwa kwenye Mamlaka za Serikali ya Mitaa zote kwa gharama ya **Shilingi bilioni 50.78**. Ntoa rai kwa Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau wengine kuendelea kuimarisha vitalu vya miche na kupanda miti ya kutosha ili kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi.

## **Utawala Bora na Usimamizi wa Rasilimali**

- 95. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka

za Serikali za Mitaa na maeneo yaliyopatiwa kipaumbele ni kama ifuatavyo:

**Ushughulikiaji wa Kero na Malalamiko ya Wananchi Katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

- 96. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuimarisha uratibu wa madawati ya malalamiko na kero katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, jumla ya malalamiko **787** yalipokelewa kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali. Kati ya malalamiko hayo, **508** yalifanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi na malalamiko **279** yanaendelea kufanyiwa kazi kupitia Kamati zilizoundwa katika Mikoa na Halmashauri chini ya usimamizi wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri. Aidha, Viongozi wa Kitaifa, Mikoa na Wilaya wameendelea kufanya ziara na kupitia ziara hizo wamesikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

**97. Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuimarisha utendaji na uwajibikaji wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutekeleza dhana ya TAMISEMI ya Wananchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeanzisha Kituo cha Huduma ya Mawasiliano kwa Mteja (Contact Centre) chenye mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi bila ya kuhitajika kufika katika ofisi zetu. Kituo hiki kimewezeshwa na mifumo na miundombinu inayosaidia wananchi kuwasiliana na Ofisi kwa njia mbalimbali za mitandao ya kijamii, kupiga simu, kutuma ujumbe mfupi na kupata ufafanuzi, majibu, na utatuzi wa masuala yanayowakabili. Huduma hii imesaidia kutoa huduma kwa haraka na kwa gharama nafuu kwa wananchi wote na kuwezesha Viongozi wa Wizara kujua namna jamii inavyohudumiwa. Hadi Februari 2021, Kituo hiki kimeweza kuhudumia jumla ya wananchi **7,443** tangu kilipoanza kutoa huduma tarehe 06 Agosti, 2020.

**98. *Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kuongeza kasi ya kutatua kero na kushughulikia malalamiko ya wananchi katika masuala ya kisheria ambapo itashirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanzisha utaratibu maalumu wa kuwatumia Wanasheria wa Serikali walioko katika Wilaya na Mikoa kushughulikia kero na malalamiko na kuyatafutia ufumbuzi, ikiwemo kuzishauri ipasavyo Mamlaka mbalimbali za Serikali.

### **Usimamizi wa Fedha Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**99. *Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa fedha kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Miongozo inayotolewa mara kwa mara ili kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kuhakikisha kazi zinazotekelezwa zinalingana na thamani ya fedha iliyotumika. Aidha, taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa makusanyo ya Mapato ya Ndani katika Halmashauri

zote imeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari kila robo mwaka.

**100. Mheshimiwa Spika,** taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20 imebainisha kwamba Halmashauri **124** sawa na **asilimia 67** zimepata **Hati Zinazoridhisha (Hati Safi)**, Halmashauri **53** sawa na asilimia **29** zimepata **Hati Zenye Shaka** na Halmashauri **8** sawa na asilimia **4** zimepata **Hati Zisizoridhisha (Hati Chafu)**. Matokeo haya ya ukaguzi yanaonesha kutofanya vizuri kwa Halmashauri nyingi ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2018/19 ambapo Halmashauri zilizopata **Hati Zinazoridhisha** zilikuwa **176** sawa na asilimia **95** na **Hati Zenye Shaka** Halmashauri **9** sawa na asilimia **5**. Hapakuwepo na Halmashauri zilizopata **Hati Chafu**.

**101. Mheshimiwa Spika,** kufuatia matokeo hayo yasiyoridhisha, Ofisi ya Rais –

TAMISEMI itafanya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri zote zilizopata Hati Chafu na Hati zenye Shaka kubainisha sababu za matokeo hayo na kuchukua hatua stahiki za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote watakaothibitika kuwa chanzo cha kutofanya vizuri kwa Halmashauri zao.

**102. *Mheshimiwa Spika***, pamoja na hoja ambazo zimesababisha hati mbaya na hati zenye shaka katika Hesabu za Halmashauri, Taarifa ya CAG imebainisha hoja nyingine ambazo hazikutajwa kwenye hati mbaya au hati zenye shaka ambazo tumebaini kuwa hoja hizo ni muhimu kufuatiliwa kwa karibu. Hivyo, Ofisi ya Rais TAMISEMI itazifuatilia na kuzisimamia Halmashauri zote ili kuhakikisha kwamba masuala yote yaliyobainishwa na CAG yanafanyiwa kazi kikamilifu ikiwemo kuchukua hatua kwa watumishi wote wa Halmashauri ambao hawakutekeleza majukumu yao ipasavyo au kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu wa fedha za umma.

## **Ununuzi wa Magari ya Viongozi wa Mikoa na Halmashauri**

**103. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali ilitenga jumla ya **Shilingi bilioni 29.83** kwa ajili ya kununua magari **238**. Kati ya magari hayo, **16** ni kwa ajili ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na magari **38** kwa ajili ya Halmashauri **38** zenye makusanyo madogo ya Mapato ya Ndani ambapo kwa mapato hayo hazina uwezo wa kumudu gharama za ununuzi wa magari. Aidha, magari **184** ni kwa ajili ya Halmashauri **184** ili kuwezesha na kurahisisha utendaji wa Idara za Elimu katika Halmashauri yamenunuliwa. Vilevile, magari **43** yametolewa na Serikali kutoka Taasisi mbalimbali kwa ajili ya Wakuu wa Wilaya ili kusaidia utendaji katika ofisi za Wakuu wa Wilaya. Hadi Februari, 2021 jumla ya magari **194** yamenunuliwa yakiwemo magari manne **(4)** kwa ajili ya Makatibu Tawala wa Mikoa ya Mtwara, Simiyu, Njombe na Kagera, gari



moja **(1)** la Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, magari matano **(5)** kwa ajili ya Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya za Bukombe, Rufiji, Butiama, Itigi na Halmashauri ya Mji wa Bunda.

### **Uendelezaji Miji na Vijiji**

**104. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta katika kuandaa na kutekeleza mipango ya Uendelezaji wa Vijiji na Miji nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri za Miji ya Geita, Njombe na Tunduma zimekamilisha uandaaji wa Mipango Kabambe ya Uendelezaji Miji. Mipango hiyo inaandaliwa kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta kwa lengo la kuwa na mipango ya pamoja ili utekelezaji wake uwe shirikishi na wenye tija. Aidha, mipango hiyo inasaidia katika uboreshaji wa miundombinu ya masoko, vituo vya mabasi na malori, madampo ya kisasa, viwanda vidogo na vya kati, maduka

makubwa, afya, elimu, maji, umeme na barabara.

**105. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea na usimamizi wa utekelezaji wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Mwongozo wa Mwaka 2018. Hadi Februari, 2021 kati ya maombi **7,161** yaliyopokelewa, vibali **5,497** vilitolewa sawa na **asilimia 76.76**. Aidha, ukaguzi umeimarishwa ili kuleta ubora wa ujenzi.

**106. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Halmashauri zililenga kukusanya **Shilingi billioni 7.06** kutokana na ada ya vibali vya ujenzi. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi billioni 3.54** sawa na **asilimia 50.1** ya lengo zimekusanywa. Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi umesaidia kupunguza ujenzi holela, urasimu, muda wa kutoa vibali na kuongeza mapato ya Serikali. Katika mwaka ujao wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatarajia kukamilisha uandaaji wa mfumo

wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya ujenzi pamoja na kuimarisha utekelezaji wa Mwongozo wa Anwani za Makazi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**107. *Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Mfumo wa Taarifa za Kijiografia (Geographical Information System - GIS) imekamilisha uandaaji wa Ramani Mnato za maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya na Halmashauri. Ramani mnato husaidia katika kuonyesha hali halisi ya mtawanyiko wa huduma za kiuchumi na kijamii kama vile minara ya simu, barabara, umeme, uoto wa asili, shule, hospitali na maji. Kazi hiyo imefanyika kwa kushirikisha Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Aidha, katika kuonesha mwenendo wa ukuaji wa miji nchini, kanzidata ya viashiria vya ukuaji wa miji imeandaliwa ambayo itawezesha utekelezaji wa mipango ya uendelezaji wa Miji nchini hususan Miji Midogo inayochipukia.

## **Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA**

**108. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki na miundombinu ya TEHAMA kwenye Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake na vituo vya kutolea huduma ambapo imeongeza ufanisi na uwajibikaji. Mifumo mbalimbali imefanyiwa usanifu na kujengwa kwenye maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imewezesha mifumo kutumika kwenye vituo **26,939** vya kutolea huduma ambavyo ni Shule za Msingi, Shule za Sekondari, Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati.

**109. Mheshimiwa Spika,** Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Takwimu za Elimumsingi (BEMIS) ambao umeimarishwa kwa kujengewa Mfumo wa Maombi ya Ajira za Walimu (OTEAS), Mfumo wa Taarifa za kila siku za Usimamizi na Uendeshaji wa Shule (SIS), Mfumo wa Usajili na

Uandikishaji wa Wanafunzi (PReM/PReMs) na Mfumo wa Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi (Students' Selection MIS).

**110. *Mheshimiwa Spika***, Mifumo mingine ambayo Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia ni Mfumo wa Kuandaa Mipango, Bajeti na Utoaji Wa Taarifa (PlanRep); Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na Utoaji wa Taarifa za Kihesabu kwa ngazi ya Kituo (FFARS); Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCS); Mfumo wa Kuratibu zoezi la Upangishaji wa maeneo ya Biashara kwenye Miradi ya Kimkakati (PANGISHA); Mfumo wa Uendeshaji wa Tovuti za Serikali (GWF); Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Shughuli za Vituo vya Kutolea Huduma za Afya (GoTHOMIS); Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma (Epicor) ambao kuanzia Julai Mosi, utaondolewa na kuanza kutumia Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE).

**111. *Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya kuwasilisha kwa wakati kumbukumbu za madeni ya watumishi hasa walimu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesanifu na kusimika Mfumo wa Kuratibu Madai na Madeni ya Watumishi (MADENI-MIS) kwa lengo la kumrahisishia mtumishi kuanzisha na kufuatilia ombi lake la madai na madeni. Mfumo huu utaunganishwa na Mfumo wa Serikali wa Madeni (GAMS).

**112. *Mheshimiwa Spika***, matumizi ya mifumo hii ya kielekroniki imeendelea kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa muhimu za utendaji kutoka ngazi za vituo na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mifumo hii imewezesha kupungua kwa matumizi ya karatasi katika utendaji wa kila siku na utoaji wa taarifa, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuongeza uwazi na uwajibikaji, utunzaji wa kumbukumbu; ushirikishwaji wa wananchi na utoaji wa huduma kwa haraka.

**D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI  
KWA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA  
RAIS-TAMISEMI**

**WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA  
MIJINI (TARURA)**

**113. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) umeendelea na utekelezaji wa majukumu ya ukarabati, matengenezo na ujenzi wa barabara na madaraja katika Halmashauri zote nchini. Wakala pia umefanya usanifu wa barabara na madaraja pamoja na kusimamia makusanyo ya ada na tozo za matumizi ya hifadhi ya barabara. Aidha, Wakala umeendelea kusimamia mtandao wa barabara wenye jumla ya **kilomita 108,946.19** ambapo **kilomita 2,250.69** ni za lami, **kilomita 27,809.26** ni za changarawe na **kilomita 78,886.25** ni za udongo. Aidha, jumla ya **kilomita 16,168.47** za mtandao wote wa barabara sawa na **asilimia 15** upo kwenye hali nzuri,

**kilomita 39,027.62** sawa na **asilimia 36** upo kwenye hali ya wastani na **kilomita 53,750.10** sawa na **asilimia 49** upo kwenye hali mbaya.

**114. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 275.03** kwa ajili ya ukarabati, matengenezo na ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilomita 23,402.61**, **madaraja 77**, **makalvati 271** na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua **kilomita 79.98**. Hadi Februari 2021, **Shilingi bilioni 172.85** zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia **63**. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa **kilomita 97.7** na matengenezo ya barabara zenye urefu wa **kilomita 7,757.13** ikiwa ni matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum. Aidha, **ajira 8,044** za muda na mikataba zimezalishwa katika eneo la matengenezo, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya barabara za Vijijini na Mijini kupitia TARURA.



**Mradi wa Uboreshaji wa Barabara Maeneo  
ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (EU-  
Agriconnect Project)**

**115. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) inaendelea na ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa **kilomita 87.6** katika Halmashauri za Wilaya ya Mufindi, Kilolo, Mbeya na Rungwe kwa gharama ya **Shilingi bilioni 40.76**. Lengo la mradi huu ni kufungua barabara kwenye maeneo yenye kilimo cha mazao ya chai, kahawa na mbogamboga ili kurahisisha usafirishaji wa mazao na kuongeza soko la mazao ya kilimo. Hadi Februari 2021, fedha zote zilikuwa zimepokelewa ambazo ni **Shilingi bilioni 40.76** ambapo ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa **kilomita 12.2** umekamilika na ujenzi wa **kilomita 75.4** zilizobaki uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

## **Ujenzi wa Barabara za Mji wa Serikali Eneo la Mtumba**

**116. Mheshimiwa Spika**, Wakala unaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa **kilomita 51.2** katika Mji wa Serikali Eneo la Mtumba kwa gharama ya **Shilingi bilioni 89.11**. Mradi huu unatekelezwa ndani ya miezi **18** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2021. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 22.41** zilikuwa zimetolewa na kutumika ambapo jumla ya **kilomita 15.2** zimekamilika kwa kiwango cha lami, makalavati **83** kati ya **118** yamekamilika, boxi kalavati zote **10** zimekamilika na utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 71**.

## **Utekelezaji wa Ujenzi wa Barabara za Ahadi za Viongozi**

**117. Mheshimiwa Spika**, Wakala umeendelea kutekeleza ahadi za ujenzi wa barabara na miundombinu mingine zilizotolewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alizozitoa katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi Februari, 2021 **Shilingi bilioni 9.39** zilipokelewa na kutumika kwenye ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilomita 64** kwa kiwango cha lami na **kilomita 15** za changarawe katika Halmashauri **65** nchini. Halmashauri **22** zimekamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami **kilomita 22**. Halmashauri zilizokamilisha ujenzi ni Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Kyerwa, Bukombe, Muleba, Mpwapwa, Kongwa, Missenyi, Ruangwa, Malinyi, Busokelo, Ludewa, Madaba, Nyasa, Itigi, Kwimba, Misungwi, Songwe na Halmashauri za Miji ya Kondo, Kasulu, Makambako na Masasi na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ambapo utekelezaji wa miradi umekamilika kwa **asilimia 100**.

### **Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini**

**118. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa

fedha 2020/21, Wakala umeendelea na matayarisho ya Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii nchini, *Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities Programme (RISE)*. Mradi huu unakadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani **milioni 350** kwa kipindi cha miaka mitano (5) ambapo **Dola za Kimarekani milioni 300** ni Mkopo wa Masharti Nafuu kutoka Benki ya Dunia na **Dola za Kimarekani milioni 50** ni mchango wa Serikali ya Tanzania. Lengo la mradi ni kujenga jumla ya **kilomita 535** za barabara za lami ambapo **kilomita 400** zitajengwa kwenye Mtandao wa barabara za Wilaya na **kilomita 135** zitajengwa kwenye barabara za Mikoza katika Halmashauri za Wilaya za Mufindi, Kilolo, Iringa, Ruangwa, Handeni na Mbogwe, kufanya matengenezo ya sehemu korofi zenye urefu wa **kilomita 2,900** na matengenezo ya kawaida **kilomita 23,000** katika Barabara za Halmashauri zote na kujenga uwezo wa Wakala katika kusimamia majukumu yake. Mradi umelenga kuboresha barabara maeneo ya

Vijijini. Aidha, barabara za Mikoa (Regional Roads) zinazounganisha maeneo hayo zitajengwa kupitia TANROADS. Serikali ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Benki ya Dunia ili kupata fedha za kuwezesha utekelezaji wa mradi huu.

### **Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP)**

**119. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam (*Dar es Salaam Metropolitan Development Project - DMDP*) una vipengele vitatu vya utekelezaji ambavyo ni uboreshaji wa barabara za kipaumbele, uimarishaji barabara na miundombinu mingine maeneo ya kaya maskini na uimarishaji wa taasisi, kujenga uwezo pamoja na uperembaji wa masuala ya kiuchumi na uendelezaji Miji. Katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi ulitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 186.80** ambapo hadi Februari 2021, kiasi cha **Shilingi bilioni 104.31** kilikuwa kimetolewa. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja

na ujenzi wa barabara zenye wa **kilomita 28** kwa kiwango cha lami na kuweka taa za barabarani, kukamilisha ujenzi wa vituo viwili vya mabasi eneo la Kijichi na Mbagala Kuu, ujenzi wa masoko manne ya Kijichi, Mbagala Kuu, Kilakala na Makangarawe na ujenzi wa vizimba **12** vya kuhifadhia takangumu.

**120. Mheshimiwa Spika**, miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilomita 32**, mifereji mikubwa ya maji ya mvua (storm wáter drains) yenye urefu wa **kilomita 17.9** kwenye maeneo ya Mto Sinza, Kiboko, Gerezani, Kizinga, Bonde la Sungura, Mafuriko, Yombo, Buguruni Kisiwani, Msimbazi Tenge-Liwiti pamoja na ujenzi wa mabwawa makubwa (detention ponds) ya kuhifadhi maji ya mvua. Ujenzi wa masoko **manne (4)** ya kisasa ya Mtoni, Mbagala, Kinyerezi na Buza, ujenzi wa vituo vinne vya mabasi vya Buza, Kinyerezi, Mtoni na Mbagala.

**121. *Mheshimiwa Spika***, Mradi umenunua vifaa vya kufanyia usafi miundombinu ya barabara na mifereji ya maji ya mvua, ununuzi wa vifaa vya kudhibiti takangumu kwa Halmashauri za Manispaa za Temeke, Kinondoni na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambapo jumla ya magari **20** yamenunuliwa na kugawiwa. Aidha, yamefanyika maboresho ya mfumo wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuunganishwa na mfumo wa kijiografia wenye taarifa muhimu za vyanzo vya mapato.

## **WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA DAR ES SALAAM (DART)**

**122. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) umeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi yafuatayo: kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam; kuweka

mpangilio makini wa matumizi ya barabara kuu na ndogo kwa watumiaji wote ili kupunguza msongamano; na kuhakikisha kuwepo kwa Menejimenti ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka yenye kuleta tija na ufanisi.

**123. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala ulikadiria kukusanya mapato ya ndani jumla ya **Shilingi bilioni 4.75** kutokana na ushuru wa kutumia miundombinu, ada ya eneo la matangazo, ushuru wa vyoo na ushuru wa maegesho ya magari. Hadi Februari 2021, Wakala ulikuwa umekusanya jumla ya **Shilingi billion 2.19** sawa na **asilimia 46** ya lengo.

**124. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala umeendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Ulipaji fidia kama sehemu ya maandalizi ya Awamu ya Tatu ya mradi inayohusisha barabara za Azikiwe, Maktaba, Lindi, Shaurimoyo, Uhuru, Bibi Titi, Nyerere kutoka



katikati ya Jiji la Dar es salaam hadi Gongo la Mboto zenye urefu wa **kilomita 23.6**. Hadi Februari, 2021 malipo ya fidia ya **Shilingi bilioni 2.68** yalikuwa yamefanyika kwa wananchi **26** waliopisha mradi;

- ii) Usimamizi wa uendeshaji wa huduma za Mpito awamu ya kwanza ya Mfumo wa DART kulingana na Mkataba;
- iii) Kuimarisha ulinzi na usalama na kusimamia matengenezo ya miundombinu ya BRT kwenye vituo vikuu vitano **(5)**, vituo vidogo **27**, madaraja ya watembea kwa miguu matatu **(3)** na karakana ya Jangwani;
- iv) Kuboresha vituo vya mlisho vya Muhimbili na Mbezi kwa kujenga mabanda ya abiria;
- v) Kuendelea kushiriki katika kuratibu ujenzi wa Miundombinu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili unaohusisha barabara

za Kilwa, Kawawa, Chang'ombe, Gerezani, Sokoine, Bandari zenye urefu wa **kilomita 20.3**;

- vi) Kufanya mapitio ya usanifu wa kina ikiwemo michoro ya miradi ya Awamu ya Nne na ya Tano pamoja na kufanya uthamini wa eneo la kujenga daraja la waenda kwa miguu kwenye miundombinu ya Awamu ya Pili;
- vii) Kuendelea na kazi ya kuunda mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli kwenye mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka utakaokamilika Agosti 2021; na
- viii) Usimamizi wa mitambo ya mfumo wa kukusanya nauli katika vituo mahiri vya TEHAMA.

## **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU**

**125. *Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kutekeleza jukumu

lake la kusimamia utumishi wa walimu nchini. Hadi Februari 2021, Tume ilikuwa imepokea na kusajili rufaa **148** za walimu ambapo kati yake rufaa **111** zimetolewa uamuzi; vikao **230** vya Kisheria vya Kamati za Wilaya vimefanyika katika Wilaya **139** na kuwezesha walimu **4,575** kuthibitishwa kazini; walimu **3,770** kubadilishwa vyeo baada ya kujiendeleza kielimu na mashauri **4,010** ya kinidhamu yalitolewa uamuzi. Vilevile, ziara kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za walimu zilifanyika kwenye Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Songwe, Mwanza, Tanga, Singida na Pwani ambapo walimu **1,101** walipatiwa elimu kuhusu masuala ya ajira, nidhamu na maadili ya kazi ya ualimu.

**126. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu imeanza kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (Teachers Management Information System - TSCMIS). Mfumo utaharakisha ushughulikiaji wa masuala ya rufaa,

nidhamu na malalamiko ya walimu. Aidha, Tume imenunua kiwanja katika eneo la Chinyoya – Ntyuka Jijini Dodoma kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu.

## **CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA HOMBOLO**

### **Uendeshaji wa Mafunzo ya Muda Mrefu na Mfupi**

**127. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Serikali za Mitaa kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni: kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi; kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uendeshaji na usimamizi wa Serikali za Mitaa. Mafunzo ya muda mrefu yanatolewa katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada. Katika mwaka wa masomo 2020/21, Chuo kimedahili wanafunzi **4,984** katika ngazi ya Astashahada, wanafunzi **1,601** katika ngazi ya Stashahada na wanafunzi **53** katika ngazi ya Shahada. Hivyo, jumla

ya wanafunzi **7,224** walidahiliwa kati ya lengo la kudahili wanafunzi **7,000** sawa na ongezeko la **asilimia 3.2**.

**128. Mheshimiwa Spika**, Chuo kinaendelea kuandaa mazingira ya kuboresha mifumo, miundombinu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kuwajengea uwezo watumishi na kutengeneza mitaala ya Shahada ya Kwanza ya Maendeleo ya Jamii; Rasilimaliwatu; na Utunzaji wa Kumbukumbu. Shahada hizo zinategemea kuanzishwa katika mwaka wa masomo 2021/22. Chuo kinaendelea kujenga uwezo wa watumishi katika fani mbalimbali ambapo jumla ya watumishi **45** wapo katika mpango wa mafunzo kama ifuatavyo, Shahada ya Uzamivu **21**, Shahada ya Uzamili **18** na Shahada ya kwanza sita (**6**). Chuo kimeendelea kuwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa Viongozi na Watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kiliwezesha mafunzo ya awali ya Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa

Maendeleo (*Opportunities and Obstacles to Development - O&OD*) Ulioboreshwa katika Sekretarieti **16** za Mikoa na Halmashauri **107** ambazo hazikupata mafunzo ya awamu ya kwanza.

**129. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Serikali za Mitaa kimefanya jumla ya tafiti **19** ambazo ziko katika hatua mbalimbali za machapisho. Tafiti hizi zinafanyika katika Halmashauri, lengo likiwa ni kubaini na kutatua changamoto mbalimbali zinazokwamisha utoaji wa huduma za kijamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutoa ushauri wa kitaalam.

**130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo kwa kutumia mapato ya ndani kimeendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hadi Februari 2021, Chuo kimekamilisha ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za kufundishia kwa utaratibu wa *Force Account* ambazo zina uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa gharama ya **Shilingi milioni 282**.

## **SHIRIKA LA ELIMU KIBAHA**

**131. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Elimu Kibaha limeendelea kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake ambayo ni kupambana na maadui watatu wa maendeleo yaani Ujinga, Umaskini na Maradhi kupitia Idara na Vitengo vilivyo chini yake. Hadi Februari 2021, Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi imetoa matibabu kwa wagonjwa **82,941**, kati yao wagonjwa **76,866** walitibiwa na kuondoka na wagonjwa **6,075** walilazwa.

**132. Mheshimiwa Spika,** kutokana na Hospitali hii kuwa karibu na barabara kuu ya Morogoro – Dar es Salaam, pamoja na kuhudumia wagonjwa wa kawaida imekuwa na msaada mkubwa kwa majeruhi wa ajali za barabarani ambapo hadi Februari 2021, jumla ya majeruhi wa ajali za barabarani **710** wakiwemo wanawake **162** na wanaume **548** wamehudumiwa. Aidha, Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi imeanzisha huduma kwa watoto wachanga wanaohitaji

uangalizi wa karibu, *Neonatal Intensive Care Unit* ambayo ina uwezo wa vitanda **24** na inalaza watoto kati ya **5** hadi **11** kwa siku na huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya ambapo waraibu **49** wamesajiliwa na wanaendelea na tiba. Vilevile, mafunzo ya utabibu na uuguzi yametolewa kwa wanachuo **470** katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha.

**133. *Mheshimiwa Spika***, Shirika linasimamia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi ambacho kinatoa mafunzo ya ujasiriamali ya muda mfupi na muda mrefu. Hadi Februari 2021, jumla ya wanachuo **292** walipatiwa mafunzo katika fani za kilimo, mifugo, uashi, bomba, useremala, ushonaji, upishi, fundi magari, uundaji na ufuaji vyuma na umeme wa majumbani. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wajasiriamali **267** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za udereva, ufugaji nyuki, kuku, elimu ya kuweka na kukopa, kilimo bustani na uundaji wa vikundi ambapo kiasi cha fedha **Shilingi 120,919,951** fedha za Mapato



ya Ndani kilitumika kugharamia mafunzo hayo.

**134. *Mheshimiwa Spika***, Shirika limeendelea kutunza shamba la ng'ombe wa maziwa lenye ng'ombe **65** kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na kuuzia wananchi maziwa. Kati ya hao, ng'ombe **15** wanakamliwa kwa sasa na wanatoa lita **2,700** kwa mwezi. Vilevile, Shirika linasimamia Shule tatu za Sekondari ambazo ni Shule ya Sekondari Kibaha, Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, Shule ya Sekondari Tumbi na Shule ya Msingi Tumbi zenye jumla ya wanafunzi **2,902**.

## **SHIRIKA LA MASOKO YA KARIAKOO**

**135. *Mheshimiwa Spika***, Shirika la Masoko ya Kariakoo limeendelea kutekeleza majukumu yake ya Msingi kwa Mujibu wa Sheria kwa kutoa huduma za masoko katika Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika lilikadiria kukusanya Mapato ya Ndani

**Shilingi bilioni 4.01** kutokana na ushuru wa mazao, kodi ya pango, ada ya kutumia soko na ada ya ulinzi wa maegesho. Hadi Februari 2021, Shirika lilikuwa limekusanya **Shilingi bilioni 2.15** sawa na asilimia **54** ya lengo. Makusanyo haya yameongezeka kwa **asilimia 1.4** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/20 ambapo katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020, Shirika lilikusanya wastani wa **Shilingi bilioni 2.12**.

**136. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2021, Shirika kupitia mapato yake ya ndani limekamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa paa katika eneo la soko dogo mzunguko lilipo maeneo ya Soko la Kariakoo Mtaa wa Sikukuu. Aidha, Shirika linaendelea na kazi ya kuandaa michoro ya usanifu (detailed design) na taarifa ya upembuzi yakinifu (feasibility study) kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa soko la kisasa katika eneo la soko dogo. Vilevile, Shirika limefanikiwa kuimarisha hali ya usafi na mazingira ndani na nje ya soko kwa kutekeleza mikakati ya

uondoshaji wa takangumu na maji taka, hivyo kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa watumiaji.

## **BODI YA MIKOPO YA SERIKALI ZA MITAA**

**137. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais -TAMISEMI kupitia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) imeendelea kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, Halmashauri sita (6) ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Halmashauri ya Mji wa Mbinga na Halmashauri za Wilaya za Mbinga, Tunduru, Ruangwa na Kishapu kati ya Halmashauri 11 zinazodaiwa zimerejesha sehemu ya mikopo yake yenye thamani ya **Shilingi milioni 337.66** kati ya **Shilingi bilioni 3.99**. Aidha, Bodi imeendelea kukusanya michango ya akiba kwa mujibu wa Sheria ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 55.38** kimekusanywa

kati ya **Shilingi bilioni 3.91** zinazopaswa kuchangwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**E. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 KWA OFISI YA RAIS - TAMISEMI (FUNGU 56), MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAFUNGU 26) NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (FUNGU NA. 2)**

**138. *Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 umeandaliwa kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Hotuba ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyoitoa wakati wa kuzindua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 13 Novemba 2020, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti

kwa mwaka wa fedha 2021/22, maelekezo ya Viongozi wengine wakuu wa Kitaifa, Sera za Kisekta, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati iliyohuishwa ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Fungu 56, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) na Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) kwa kipindi cha 2021/22-2025/26.

### **Ofisi ya Rais –TAMISEMI (Fungu 56)**

**139. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

- i) Utoaji wa Huduma bora za Afya ya Msingi ikijumuisha ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba pamoja na ujenzi wa miundombinu ya zahanati, vituo vya afya na Hospitali za Halmashauri;
- ii) Utoaji wa Huduma bora za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa kununua vitabu, vifaa vya maabara

pamoja na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, maabara, nyumba za walimu, Shule za Sekondari za sayansi za wasichana, ujenzi wa shule za kutwa za Kata pamoja na utengenezaji wa madawati kwa Shule za Msingi;

- iii) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za Vijijini na Mijini;
- iv) Kuwawezesha wananchi kiuchumi; na
- v) Kuimarisha Utawala bora na usimamizi wa rasilimali; na
- vi) Kujenga mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji wa viwanda Mijini na Vijijini.

**140. *Mheshimiwa Spika***, kupitia Vipaumbele hivi, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:

- i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatujaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

- ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma ya Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo;
- iv) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- v) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;
- vi) Kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa lengo la kuongeza ufanisi;
- vii) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa

uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;

- viii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya Ukaguzi, Ufuatiliaji na Tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, Programu na Miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ix) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni pamoja na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- x) Kuratibu shughuli za utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;



- xi) Kuratibu usafiri na usafirishaji, ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara, afya na elimu inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xii) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, Halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri **30** ambazo zimehamia katika maeneo yake ya utawala;
- xiii) Kusimamia matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na
- xiv) Kuratibu uendelezaji wa Vijiji na Miji na kuimarisha utangamano wa Vijiji na Miji (Rural–Urban Intergration).

### **Tawala za Mikoa (Mafungu 26)**

**141. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Tawala za Mikoa zimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;
- ii) Kuratibu utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan katika usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, lishe na ustawi wa jamii;
- iii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa majengo ya Ofisi na nyumba za makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Makatibu Tawala Wasaidizi, Maafisa Tarafa na Maafisa Waandamizi;
- iv) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Sera ya Ukatuaji wa Madaraka kwa Wananchi na Sera nyingine za kisekta ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi;
- v) Kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali fedha katika Mikoa na

- Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi) Kuratibu na kufanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
  - vii) Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
  - viii) Kuratibu uanzishwaji wa viwanda kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara Mijini na Vijijini, uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa na kuhimiza shughuli za kuongeza mnyororo wa thamani katika bidhaa zinazozalishwa na wananchi;
  - ix) Kutatua migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
  - x) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika kuimarisha uchumi kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
  - xi) Kusimamia na kuimarisha Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na

- Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xii) Kuratibu uanzishaji wa viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, misitu, mifugo na uvuvi;
  - xiii) Kufanya mapitio ya Mipango Mikakati ya Sekretarieti za Mikoa na kuratibu mapitio ya Mipango Mikakati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
  - xiv) Kuratibu uendelezaji wa maeneo maalum ya shughuli za kiuchumi na uwekezaji;
  - xv) Kuratibu utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake (**asilimia 4**), Vijana (**asilimia 4**) na Watu Wenye Ulemavu (**asilimia 2**);
  - xvi) Kuhamasisha na kusimamia kilimo cha mazao ya kimkakati ambayo ni Korosho, Chai, Tumbaku, Katani, Kahawa, Pamba na Michikichi; na
  - xvii) Kuhamasisha uwekezaji katika maeneo yao ya utawala.

## **Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 ndani ya Mafungu 26 ya Mikoa**

**142. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/22, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji kwa kuhakikisha mikutano ya kisheria inafanyika na taarifa za mikutano hiyo zinawekwa katika maeneo ya wazi na katika tovuti za kila Halmashauri hasa taarifa za mapato na matumizi.
- ii) Kuimarisha na kubuni mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ikiwemo mapato ya kodi ya majengo na ushuru wa mabango;
- iii) Kusimamia ulinzi na usalama;
- iv) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi katika sekta zote hususan kujenga na

- kuboresha Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati, vyumba vya maabara za sayansi katika Shule za Sekondari, nyumba za watumishi, matundu ya vyoo, na vyumba vya madarasa;
- v) Kusimamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo katika Shule za Msingi na Sekondari;
  - vi) Ukamilishaji na kuanza ujenzi wa majengo ya Ofisi, nyumba za makazi ya Viongozi na watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo Halmashauri 30 zilizohamia katika maeneo yake ya utawala;
  - vii) Kukamilisha ujenzi wa miradi viporo ya miundombinu mbalimbali ya huduma za kijamii;
  - viii) Kubuni, kuandaa maandiko na kutekeleza Miradi ya Kimkakati itakayosaidia kuongeza Mapato ya Ndani ya Halmashauri;
  - ix) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuimarisha

- utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- x) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa na maeneo ya Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo;
  - xi) Kusimamia shughuli za uendelezaji Miji na Vijiji; na
  - xii) Kusimamia utunzaji wa mazingira na shughuli mtambuka.

**F. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

**Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)**

**143. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/22, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza yafuatayo:

- i) Kupokea, kusajili na kuchambua rufaa za walimu;
- ii) Kuzijengea uwezo Ofisi za Wilaya

- 139 za Tume katika masuala ya usimamizi wa rasilimaliwatu;
- iii) Kuandaa Mwongozo wa masuala ya ajira na nidhamu;
  - iv) Kufanya mikutano na wadau kuhusu masuala ya ajira, maadili, nidhamu na maendeleo ya walimu;
  - v) Kufanya tathmini kuhusu upangaji wa walimu mashuleni na kuwezesha Ofisi za Tume katika ngazi ya Wilaya kuhuisha Tange ya Walimu;
  - vi) Kuandaa na kuratibu Mikutano sita (6) ya Tume na Vikao vinne (4) vya Kamati tatu (3) za Tume; na
  - vii) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Tume Makao Makuu Jijini Dodoma.

### **Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

**144. *Mheshimiwa Spika***, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) katika mwaka wa fedha 2021/22 utaendelea kutekeleza kazi mbalimbali za matengenezo, ukarabati na ujenzi wa barabara na madaraja kwa



kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Mpango Mkakati wa Wakala wa mwaka 2021/22 – 2025/26.

**145. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais- TAMISEMI itatoa Mwongozo kwa Halmashauri zenye mapato makubwa namna ya kuchangia fedha za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kwa TARURA. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaweka utaratibu wa mahusiano kati ya Halmashauri na TARURA ili kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi na ushirikishwaji wa Halmashauri wakiwemo Waheshimiwa Madiwani.

### **Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara na Madaraja**

**146. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo;

- i) Matengenezo ya barabara za Vijijini na Mijini zenye urefu wa **kilomita 24,630.42** ambapo **kilomita 16,300.22** ni matengenezo ya kawaida, **kilomita 5,341.82** ni matengenezo ya maeneo korofi na **kilomita 2,988.38** ni matengenezo ya muda maalum;
- ii) Ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa **kilomita 136.82**;
- iii) Ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa **kilomita 469.16**;
- iv) Ujenzi wa madaraja **93** na ukarabati wa madaraja **27**;
- v) Ujenzi wa makalavati **206** na matengenezo ya makalavati **197**; na
- vi) Ujenzi wa mifereji yenye urefu wa **kilomita 62.7**.

**Mradi wa Uboreshaji wa Barabara katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (Agri-Connect Programme)**

**147. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kutafuta fedha za

matengenezo ya barabara za Vijijini na Mijini kupitia TARURA. Katika mwaka wa fedha 2021/22, TARURA itatetekeleza mradi huu ambao unalenga kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya mbogamboga, chai na kahawa ili kuimarisha mnyonyoro wa thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko.

**148. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu utatekelezwa katika Mikoa ya Njombe, Ruvuma, Songwe, Mbeya na Iringa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa ajili ya uboreshaji wa barabara maeneo ya Vijijini zenye urefu wa **kilomita 40.00** kwa kiwango cha lami.

**Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP)**

**149. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/22, Programu ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP) itakamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilomita 16** kwa

kiwango cha lami; mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa **kilomita 17.9** pamoja na ujenzi wa masoko manne (4) ya Mtoni, Mbagala, Kinyerezi na Buza.

**Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE)**

**150. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii nchini, *Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities Programme (RISE)*. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka wa fedha 2021/22. Lengo la mradi ni kujenga jumla ya **kilomita 535** za barabara za lami ambapo **kilomita 400** zitajengwa kwenye Mtandao wa barabara za Wilaya na **kilomita 135** zitajengwa kwenye barabara za Mikoa.

**151. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mradi wa RISE, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA inatarajia kulipa fidia, kufanya upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina wa **kilomita 468** katika Mikoa ya Lindi, Tanga na Geita na kuendelea na utekelezaji wa ujenzi wa barabara za lami katika Halmashauri za Wilaya za Kilolo, Mufindi na Iringa.

### **Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART)**

**152. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umepanga kutumia **Shilingi bilioni 7.27** kama Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 1.80** ni Mishahara na **Shilingi bilioni 5.46** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha za Matumizi Mengineyo, **Shilingi milioni 696.39** ni fedha kutoka Serikali Kuu na **Shilingi bilioni 4.76** ni fedha za Mapato ya Ndani.

**153. Mheshimiwa Spika**, Wakala umepanga kuteleleza majukumu yafuatayo:

- i) Kujenga kituo cha kibiashara cha uwekezaji Gerezani - Kariakoo ili

- kuongeza mapato ya Wakala;
- ii) Kusimika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli (AFCS) na Mfumo wa kuongoza mabasi (ITS) itakayoleta huduma bora ya usafiri;
  - iii) Kuendelea na usimamizi wa uendeshaji wa huduma za mpito awamu ya kwanza ya Mfumo wa DART katika kipindi hiki kulingana na Mkataba;
  - iv) Kuendelea na usimamizi wa matengenezo ya miundombinu katika BRT awamu ya kwanza kwenye vituo vikuu vitano **(5)**, vituo vidogo **27** na madaraja matatu **(3)** ya waenda kwa miguu;
  - v) Kuimarisha usafi, ulinzi na usalama katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka awamu ya kwanza kwenye vituo vikuu vitano **(5)**, vituo vidogo **27**, madaraja matatu **(3)** ya waenda kwa miguu pamoja na karakana ya Jangwani;

- vi) Kuendelea kushiriki katika kuratibu ujenzi wa miundombinu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka awamu ya pili unaohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Chang'ombe, Gerezani, Sokoine, Bandari zenye urefu wa **kilomita. 20.30**; na
- vii) Kuendelea kufanya mapitio ya usanifu wa kina ikiwemo michoro ya miradi ya awamu ya sita.

### **Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo**

**154. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Chuo cha Serikali za Mitaa kinatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kudahili wanafunzi wapya **7,000**;
- ii) Kuendeleza na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa kozi za muda mrefu pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi yenye kuzingatia uhitaji;
- iii) Kuanzisha mafunzo ya kozi tatu za Shahada katika fani za Maendeleo ya Jamii; Menejimenti ya

- Rasilimaliwatu; na Utunzaji Nyaraka na Kumbukumbu;
- iv) Kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa;
  - v) Kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Mikutano Hombolo;
  - vi) Kujenga ukumbi wa kufundishia wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **400**;
  - vii) Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala awamu ya pili; na
  - viii) Kuendelea na ujenzi wa kumbi za kufundishia na ofisi ya Kampasi ya Dodoma mjini.

### **Shirika la Elimu Kibaha**

**155. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika la Elimu Kibaha linatarajia kutekeleza yafuatayo:

- i) Kuendelea kutoa huduma za afya za kinga na tiba katika Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi;



- ii) Kuendelea kutoa elimu ya uuguzi na utabibu katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;
- iii) Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari na Msingi;
- iv) Kuendelea kutoa huduma za maktaba;
- v) Kutoa mafunzo ya ufundi, ujasiriamali, kilimo na mifugo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha;
- vi) Kuongeza uzalishaji wa maji tiba kwa ajili ya matumizi ya Hospitali kutoka chupa **36,000** hadi chupa **72,000** kwa mwaka; na
- vii) Kuendeleza mradi wa upanuzi wa Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi kwa kukamilisha jengo litakalokuwa na wodi ya upasuaji yenye vitanda **248**, huduma za dharura, chumba cha upasuaji na ofisi za utawala.

## **Shirika la Masoko ya Kariakoo**

**156. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika la Masoko ya Kariakoo limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Shirika ili kuendana na mazingira ya sasa ya kibiashara;
- ii) Kuendelea na ujenzi wa soko la jumla katika eneo la Makonde -Mbezi Beach;
- iii) Kujenga maduka mapya **30** katika eneo la Tabata Bima;
- iv) Kufanya maboresho (Partitioning) katika duka namba G/039 katika jengo la Soko Kuu kwa kujenga maduka madogo nane (**8**);
- v) Kuendelea na ukarabati wa miundombinu chakavu katika maeneo mbalimbali; na
- vi) Kuendelea kusimamia usalama wa soko na shughuli za usafi wa mazingira na uondoshaji wa takangumu na maji taka.

## **Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**157. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kukamilisha marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Bodi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa Bodi;
- ii) Kuboresha muundo wa Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi;
- iii) Kupokea, kuchambua na kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo; na
- iv) Kufanya ufuatiliaji wa urejeshwaji wa mikopo na uwasilishwaji wa michango kutoka Halmashauri

zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi.

**MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA  
KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA  
FEDHA 2021/22**

**158. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza malengo mahsusni yafuatayo:

- i) Kuimarisha na kuhakikisha vituo vya kutolea huduma vilivyokamilika vinaanza kutoa huduma za Afya na Elimu ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba na utengenezaji wa madawati kwa Shule za Msingi na Sekondari;
- ii) Kujenga vituo vya afya vipya **121** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 60.50** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (***Rejea Kiambatisho Na. 11***);
- iii) Kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya **52** kwa gharama ya **Shilingi bilioni**

- 15.60** vilivyoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa kutumia fedha za ndani; (***Rejea Kiambatisho Na. 11***);
- iv) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali za Halmashauri **68** za awamu ya kwanza zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2018/19 ikiwemo Hospitali ya Uhuru iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 55.70** fedha za ndani zimetengwa (***Rejea Kiambatisho Na. 12***);
- v) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali **27** za awamu ya pili zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/20 na Hospitali nne (4) za awamu ya kwanza ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 11.40** fedha za ndani zimetengwa (***Rejea Kiambatisho Na. 12***);
- vi) Kuanza ujenzi wa Hospitali mpya **28** katika Halmashauri ambazo hazina Hospitali za Serikali ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 14.00** fedha za ndani

- zimetengwa (***Rejea Kiambatisho Na. 12***);
- vii) Ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali **31** za awamu ya pili ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 12.30** fedha za ndani zimetengwa (***Rejea Kiambatisho Na. 12***);
- viii) Ukamilishaji wa maboma ya zahanati **763** yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika Majimbo yote ya Uchaguzi yatakayogharimu **Shilingi bilioni 38.15** ambapo kila zahanati imetengewa **Shilingi milioni 50** (***Rejea Kiambatisho Na. 13***);
- ix) Kuanza Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa **shule 10 kati ya shule 26** za Sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya Sayansi (shule moja kwa kila Mkoa) ambayo katika Awamu hii itajengwa miundombinu ya Kidato cha Tano na Sita. Aidha, shule hizi zitakapokamilika zitakuwa na Kidato cha Kwanza hadi cha Sita na wanafunzi kati ya **1,000** hadi

- 1,200** kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 40** zimetengwa;
- x) Kujenga Shule mpya **300** za Sekondari za kutwa kwenye Kata ambazo hazina Shule za Sekondari kwa gharama ya **Shilingi milioni 650 hadi 700** kwa kila shule kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP);
- xi) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba **1,840** vya madarasa ya Shule za Sekondari kwa gharama ya **Shilingi bilioni 23.00 (Rejea Kiambatisho Na. 14)**;
- xii) Kujenga nyumba **300** (Two in One) za walimu kwa gharama ya **Shilingi milioni 50** kwa kila nyumba;
- xiii) Kuendelea kugharamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 312.05** fedha za ndani zimetengwa (**Rejea Kiambatisho Na. 15**);

- xiv) Ununuzi wa vitabu vya Shule za Msingi na Sekondari kwa gharama ya **Shilingi bilioni 50.00** fedha za ndani;
- xv) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba **3,268** kwa madarasa ya Shule za Msingi kwa gharama ya **Shilingi bilioni 40.85** (*Rejea Kiambatisho Na.16*);
- xvi) Kuhakikisha upatikanaji wa madawati ya Shule za Msingi **710,000** ili kukabiliana na upungufu wa madawati **1,048,561** kwa kuanzia kiasi cha **Shilingi bilioni 6.73** kimetengwa;
- xvii) Ukamilishaji wa vyumba **1,043** vya maabara za sayansi katika Shule za Sekondari kwa gharama ya **Shilingi bilioni 26.07** - fedha za ndani (*Rejea Kiambatisho Na. 17*);
- xviii) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya Utawala ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 57.92**



- fedha za ndani zimetengwa (***Rejea Kiambatisho Na. 18***);
- xix) Ujenzi wa majengo ya Utawala kwa Halmashauri **96** kwa gharama **Shilingi bilioni 83.75** na ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara katika Halmashauri **51** ikijumuisha Halmashauri **30** zilizohamia kwenye maeneo yao ya utawala utakaogharimu **Shilingi bilioni 7.65** fedha za ndani (***Rejea Kiambatisho Na. 19***);
- xx) Ununuzi wa magari **66** kwa ajili ya Viongozi wa Mikoa na Halmashauri, kiasi cha **Shilingi bilioni 14.80** fedha za ndani zimetengwa (***Rejea Kiambatisho Na. 20***);
- xxi) Utekelezaji wa Miradi **31** ya Kimkakati katika Halmashauri **26** ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 68.70** fedha za ndani kimetengwa (***Rejea Kiambatisho Na. 21***);
- xxii) Utoaji wa mikopo ya **asilimia 10** kwa vikundi vya Wanawake, Vijana

na Watu Wenye Ulemavu kupitia Mapato ya Ndani ya Halmashauri ambapo **Shilingi bilioni 67.66** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 22*);

- xxiii) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kwa gharama ya **Shilingi bilioni 627.044** kupitia TARURA ambapo **Shilingi bilioni 272.50** zinatokana na Mfuko wa Barabara, **Shilingi bilioni 127.50** zinatokana na Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 12.75** zinatokana na Mapato ya Ndani ya TARURA ambapo jumla ya **kilomita 136.82** barabara za lami, **kilomita 500** za barabara za changarawe na Kalvati/madaraja **90** yatatengenezwa. Aidha, kiasi cha **Shilingi bilioni 214.294** ni fedha za nje ambapo **Shilingi bilioni 156.031** ni kwa ajili ya kuendeleza miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam na kiasi cha **Shillingi bilioni 22.263** ni fedha za Mradi wa Uboreshaji wa Barabara

Maeneo ya Uzalishaji wa Kilimo (EU – Agriconnent Project) pamoja na **Shilingi bilioni 36.00** ni Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (Roads to Inclusion and Socio Economic Opportunities Programme - RISE). Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa **kilomita 91** kwa kiwango cha lami maeneo ya Vijijini, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua **kilomita 17.9**, ujenzi wa masoko manne (4), kulipa fidia, na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya matengenezo ya barabara **kilomita 468**;

## **G. SHUKRANI**

**159. Mheshimiwa Spika;** kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, naomba kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi

imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Humphrey Hezron Polepole (Mb), Mwenyekiti wa Kamati, na Makamu wake Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo (Mb), kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Maoni na ushauri wa Kamati vimesaidia kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**160. Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hao wa Maendeleo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya

Ulaya (EU), *Global Partnership for Education*, Shirika la Maendeleo la Uingereza (Foreign, Commonwealth and Development Office-FCDO), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Nchi zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya ambazo ni Denmark, Ireland, Jamhuri ya Korea (KOICA) na Switzerland.

**161. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa Miradi na Programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sehemu kubwa ya mafanikio ambayo Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepata katika uboreshaji huduma za afya, elimu

na sekta nyingine za kiuchumi na kijamii yametokana na ushirikiano wa wananchi na Wadau mbalimbali wa Maendeleo.

**162. *Mheshimiwa Spika***, napenda kuishukuru Serikali kwa kukubali na kuweka kisheria mfumo wa ujenzi wa miundombinu kwa kutumia *Force Account* ambao umeokoa gharama kubwa na kuwezesha upatikanaji wa miundombinu mingi kwa gharama nafuu. Aidha, mfumo huu umeongeza ari ya wananchi kushiriki na kuchangia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao na hivyo kufanya miradi hiyo kuwa endelevu.

**163. *Mheshimiwa Spika***, napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kipekee, nawashukuru Naibu Mawaziri, *Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange*, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na *Mheshimiwa David Ernest Silinde*, Mbunge wa Jimbo la Tunduma, kwamsaada mkubwa wanaotoa kwangu katika kutekeleza

majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Aidha, namshukuru *Katibu Mkuu, Prof. Riziki S. Shemdoe* kwa mchango wake katika kufanikisha maandalizi ya Mpango na Bajeti na Naibu Makatibu Wakuu *Bw. Gerald G. Mveli* na *Dkt. Grace E. Magembe* katika usimamizi wa majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Vilevile, nimpongeze *Bi. Paulina Mbena Nkwama* Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuteuliwa katika nafasi hiyo. Aidha, ninawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

**164. *Mheshimiwa Spika***, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, *Mheshimiwa George Huruma Mkuchika (Mb)*, Waziri

Ofisi ya Rais Kazi Maalum, *Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (Mb)*, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe *Deogratius Ndejemi* Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais. Aidha, ninawashukuru *Dkt. Laurean Ndumbaro*, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, *Dkt. Moses Kusiluka* Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu na *Dkt. Francis Michael*, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao.

**165. *Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee, namshukuru *Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb)*, Waziri wa Fedha na Mipango, *Mheshimiwa Mhandisi Hamadi Masauni (Mb)*, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, *Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba*, Mlipaji Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu



Wizara ya Fedha na Mipango na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao wanaoutoa katika maandalizi na utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**166. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**167. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Tanga Mjini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2020 na hivyo kuniwezesha kuweka historia ya kuwa Mbunge wa kwanza Mwanamke wa Jimbo hili toka lilipoanzishwa mwaka 1965. Ninawaahidi wana Tanga Mjini kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu

zangu zote ili kuifanya Tanga yetu ipate maendeleo zaidi ya kiuchumi na kijamii. Kipekee, ninaishukuru familia yangu kwa kuniombea na kwa uvumilivu wao muda wote ninapokuwa mbali nao katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa.

## **H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

### **Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani**

**168. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoja **26** na Halmashauri **184** inaomba idhini ya kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Tisa Kumi na Sita Milioni Mia Nne na Arobaini na Tano Mia Nne na Tisa Eflu Mia Moja Tisini na Nane (Shilingi 916,445,409,198)**, makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, ada za wanafunzi, tozo na

ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa mwaka wa fedha 2021/22**

<b>OFISI/TAASISI</b>	<b>MAKADIRIO</b>
Ofisi ya Rais – TAMISEMI	4,500,000.00
Taasisi	52,362,225,886.00
Mikoa	220,683,312.00.00
Halmashauri	863,858,000,000.00
<b>JUMLA KUU</b>	<b>916,445,409,198.00</b>

**169. Mheshimiwa Spika;** sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22 jumla ya **Shilingi Trilioni Saba Bilioni Mia Sita Themanini na Tatu Milioni Mia Tatu Ishirini na Tisa Mia Sita Arobaini na Nne Elfu na Mia Nane**

**(Shilingi 7,683,329,644,800.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu **56**, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. **2** na Mafungu **26** ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri **184**.

**170. Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha zinazoombwa, **Shilingi 4,728,008,207,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara **Shilingi 3,972,149,603,000.00** na **Shilingi 755,858,604,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,955,321,437,800.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 1,676,459,779,800.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,278,861,658,000.00** ni fedha za nje (*Mchanganuo wa fedha zinazoombwa katika mwaka wa fedha 2021/22 umeoneshwa katika Jedwali Na. 2 na Kiambatisho Na. 23, 24, 25 na 26*).

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Makisio katika Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/22**

<b>AINA YA MATUMIZI</b>	<b>BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22</b>
<b>Matumizi ya Kawaida Ofisi ya Rais -TAMISEMI</b>	
<b>Mishahara</b>	
Mishahara Makao Makuu	10,278,507,000.00
Mishahara ya Taasisi	47,235,991,000.00
<b>Jumla Mishahara Ofisi ya Rais - TAMISEMI</b>	<b>57,514,498,000.00</b>
<b>Matumizi Mengineyo</b>	
Makao Makuu	10,054,284,000.00
Taasisi	1,318,870,000.00
<b>Jumla ya Matumizi Mengineyo</b>	<b>11,373,154,000.00</b>
<b>Jumla Matumizi ya Kawaida</b>	<b>68,887,652,000.00</b>

<b>AINA YA MATUMIZI</b>	<b>BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22</b>
<b>TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)</b>	
Mishahara	7,760,568,000.00
Matumizi Mengineyo	6,608,202,000.00
<b>Jumla ya Matumizi ya Kawaida TSC</b>	<b>14,368,770,000.00</b>
<b>MIKOA NA HALMASHAURI</b>	
<b>MIKOA:</b>	
Mishahara	71,269,064,000.00
Matumizi Mengineyo	57,449,078,000.00
<b>Jumla ya Matumizi ya Kawaida</b>	<b>128,718,142,000.00</b>
<b>HALMASHAURI</b>	
Mishahara	3,835,605,473,000.00
Matumizi Mengineyo (SK)	147,659,832,000.00
Matumizi Mengineyo (MSM)	532,768,338,000.00
<b>Jumla Matumizi ya Kawaida</b>	<b>4,516,033,643,000.00</b>
<b>MIRADI YA MAENDELEO</b>	
OFISI YA RAIS -TAMISEMI	
Fedha za Ndani	451,506,768,800.00

<b>AINA YA MATUMIZI</b>	<b>BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22</b>
Fedha za Nje	199,836,336,000.00
<b>Jumla Maendeleo</b>	<b>651,343,104,800.00</b>
<b>TUME YA UTUMISHI WA WALIMU</b>	
Fedha za Ndani	500,000,000.00
<b>Jumla</b>	<b>500,000,000.00</b>
<b>MIKOA</b>	
Fedha za Ndani	62,942,998,000.00
Fedha za Nje	21,548,505,000.00
<b>Jumla Maendeleo</b>	<b>84,491,503,000.00</b>
<b>HALMASHAURI</b>	
Fedha za Ndani (SK)	830,420,351,000.00
Fedha za Ndani (MSM)	331,089,662,000.00
Fedha za Nje	1,057,476,817,000.00
<b>Jumla Maendeleo Halmashauri</b>	<b>2,218,986,830,000.00</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>7,683,329,644,800.00</b>

**SK** – Serikali Kuu na **MSM** – Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

**171. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa

kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu **56**), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. **2**), Mikoa na Halmashauri (Mafungu **26**) ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

**172. Mheshimiwa Spika,** hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)

**173. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja









**Kiambatisho Na. 1**

**MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA 2019/20, 2020/21 HADI FEBRUARI NA MAKISIO YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

NA.	Mkoa/ Halmeshauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa Fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
	<b>Katavi</b>									
1	Mpanda MC	2,486,100,620	2,968,914,746	119	2,627,606,000	1,739,087,211	66	3,254,000,000	1,035,000,000	2,219,000,000
2	Tanganyika DC	3,177,384,000	3,069,250,838	97	3,194,167,656	2,405,268,448	75	5,574,000,000	1,511,000,000	4,063,000,000
3	Nsimbo DC	821,717,684	993,700,090	121	1,247,386,808	840,356,422	67	1,191,000,000	400,000,000	791,000,000
4	Mlele DC	990,982,285	704,690,498	71	869,043,900	682,974,370	79	957,000,000	320,000,000	637,000,000
5	Mpimbwe DC	1,617,208,000	1,504,162,722	93	1,376,595,000	1,116,316,363	81	1,608,000,000	542,000,000	1,066,000,000
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>9,093,392,589</b>	<b>9,240,718,894</b>	<b>102</b>	<b>9,314,799,364</b>	<b>6,784,002,814</b>	<b>73</b>	<b>12,584,000,000</b>	<b>3,808,000,000</b>	<b>8,776,000,000</b>
	<b>Simiyu</b>									
6	Bariadi TC	2,244,992,240	1,923,882,495	86	1,759,350,000	1,280,737,052	73	3,324,000,000	1,023,000,000	2,301,000,000
7	Bariadi DC	1,752,000,000	1,180,059,814	67	4,174,403,651	1,154,667,297	28	1,851,000,000	656,000,000	1,195,000,000

NA.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
8	Maswa DC	3,235,525,000	1,836,489,073	57	3,395,561,002	1,386,410,804	41	2,252,000,000	623,000,000	1,628,000,000
9	Meatu DC	2,135,366,000	1,626,286,163	76	2,476,736,848	1,728,685,676	70	2,574,000,000	872,000,000	1,701,000,000
10	Busega DC	1,920,500,000	1,308,228,765	68	2,345,145,305	905,551,692	39	2,064,000,000	691,000,000	1,373,000,000
11	Itilima DC	1,716,495,052	1,005,880,187	59	1,434,558,653	451,597,530	31	1,487,000,000	445,000,000	1,042,000,000
	<b>Jumlia ndogo</b>	<b>13,004,878,292</b>	<b>8,880,826,497</b>	<b>68</b>	<b>15,585,755,458</b>	<b>6,907,649,990</b>	<b>44</b>	<b>13,552,000,000</b>	<b>4,310,000,000</b>	<b>9,240,000,000</b>
	<b>Njombe</b>									
12	Njombe TC	3,300,000,000	5,608,630,932	170	6,704,334,000	4,937,190,886	74	6,717,000,000	1,905,000,000	4,811,000,000
13	Makambako TC	2,553,910,000	2,458,943,255	96	2,878,062,000	1,736,313,600	60	3,228,000,000	1,140,000,000	2,088,000,000
14	Njombe DC	1,989,657,013	2,924,217,325	147	2,373,998,200	2,315,537,765	98	2,982,000,000	1,131,000,000	1,851,000,000
15	Ludewa DC	1,545,510,000	1,086,071,921	70	1,896,599,231	1,056,658,907	56	2,037,000,000	521,000,000	1,515,000,000
16	Makete DC	2,400,268,000	2,230,029,747	93	2,441,877,000	1,561,689,470	64	2,487,000,000	743,000,000	1,743,000,000
17	Wanging'ombe DC	1,263,545,000	1,318,143,411	104	2,642,402,800	1,422,015,626	54	3,489,000,000	960,000,000	2,529,000,000
	<b>Jumlia ndogo</b>	<b>13,052,890,013</b>	<b>15,626,036,591</b>	<b>120</b>	<b>18,937,273,231</b>	<b>13,029,406,254</b>	<b>69</b>	<b>20,940,000,000</b>	<b>6,400,000,000</b>	<b>14,537,000,000</b>
	<b>Geita</b>									

NA.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
18	Geita TC	6,086,158,950	9,222,763,959	152	8,795,384,709	7,687,803,063	87	10,254,000,000	5,457,000,000	4,797,000,000
19	Geita DC	3,725,257,506	4,490,280,937	121	4,078,343,000	3,597,241,189	88	4,668,000,000	1,720,000,000	2,948,000,000
20	Bukombe DC	1,990,903,000	2,390,278,702	120	1,945,991,292	852,759,993	44	3,162,000,000	923,000,000	2,239,000,000
21	Chato DC	2,996,034,000	3,642,695,020	122	3,382,577,706	1,335,816,097	39	3,996,000,000	1,048,000,000	2,948,000,000
22	Mbogwe DC	906,684,000	1,042,769,025	115	992,716,000	722,520,842	73	1,578,000,000	564,000,000	1,014,000,000
23	Nyang'hwale DC	832,190,000	1,076,533,093	129	1,505,130,145	1,158,561,335	77	1,805,000,000	521,000,000	1,284,000,000
	<b>Jumlia ndogo</b>	<b>16,537,227,456</b>	<b>21,865,320,736</b>	<b>132</b>	<b>20,700,142,852</b>	<b>15,354,702,519</b>	<b>74</b>	<b>25,463,000,000</b>	<b>10,233,000,000</b>	<b>15,230,000,000</b>
	<b>Arusha</b>									
24	Arusha CC	20,667,496,070	19,222,111,913	93	22,099,965,000	12,029,468,413	54	23,295,000,000	12,046,000,000	11,249,000,000
25	Monduli DC	2,905,000,000	2,544,992,262	88	2,677,907,654	1,057,035,763	39	2,250,000,000	575,000,000	1,675,000,000
26	Ngorongoro DC	2,365,000,000	1,563,818,669	66	2,834,646,000	891,016,184	31	2,753,000,000	893,000,000	1,860,000,000
27	Karatu DC	3,314,910,000	3,249,075,705	98	4,501,993,140	1,942,573,972	43	3,964,000,000	1,272,000,000	2,691,000,000
28	Meru DC	3,437,795,356	2,944,429,762	86	4,049,395,098	3,035,290,421	75	3,499,000,000	872,000,000	2,627,000,000
29	Arusha DC	5,073,324,560	4,092,429,940	81	4,219,639,760	2,300,010,453	55	4,383,000,000	862,000,000	3,521,000,000

NA.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
30	Longido DC	1,928,423,600	1,457,314,345	76	2,208,158,000	882,641,743	40	2,239,000,000	797,000,000	1,442,000,000
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>39,691,949,586</b>	<b>35,066,172,596</b>	<b>88</b>	<b>42,591,704,652</b>	<b>22,138,036,949</b>	<b>52</b>	<b>42,383,000,000</b>	<b>17,317,000,000</b>	<b>25,065,000,000</b>
	<b>Pwani</b>									
31	Kibaha TC	4,033,739,848	3,622,590,352	90	4,385,495,650	3,260,773,229	74	4,491,000,000	1,643,000,000	2,848,000,000
32	Bagamoyo DC	3,172,893,678	1,992,252,584	63	3,493,107,500	1,933,372,988	55	3,914,000,000	818,000,000	3,096,000,000
33	Mafia DC	1,850,448,160	1,152,641,468	62	1,720,122,583	846,264,727	49	1,680,000,000	495,000,000	1,185,000,000
34	Kisarawe DC	4,464,012,000	2,352,130,558	53	5,375,311,967	2,087,330,212	39	3,017,000,000	789,000,000	2,228,000,000
35	Kibaha DC	3,009,350,976	1,565,935,145	52	2,839,687,309	984,574,217	35	1,886,000,000	485,000,000	1,400,000,000
36	Rufiji DC	2,145,374,541	1,774,157,765	83	2,741,697,495	2,951,323,732	108	3,657,000,000	1,181,000,000	2,476,000,000
37	Mkuranga DC	6,306,413,000	6,620,512,352	105	7,180,720,000	5,091,150,265	71	7,826,000,000	2,737,000,000	5,090,000,000
38	Chalinze DC	6,167,900,000	7,110,585,005	115	8,591,450,870	6,158,040,444	72	10,728,000,000	5,717,000,000	5,010,000,000
39	Kibiti DC	2,515,427,427	1,874,463,269	75	2,367,340,780	1,375,945,168	58	2,107,000,000	733,000,000	1,374,000,000
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>33,665,559,630</b>	<b>28,065,268,498</b>	<b>83</b>	<b>38,694,934,153</b>	<b>24,688,774,981</b>	<b>64</b>	<b>39,306,000,000</b>	<b>14,598,000,000</b>	<b>24,707,000,000</b>
	<b>Dondoma</b>									

NA.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
40	Dodoma CC	72,970,496,426	53,249,433,678	73	47,104,504,276	21,191,392,017	45	50,116,000,000	28,375,000,000	21,741,000,000
41	Kondoa TC	1,636,958,528	1,417,208,831	87	1,410,160,028	867,686,778	62	1,509,000,000	317,000,000	1,192,000,000
42	Kondoa DC	1,369,678,493	1,018,560,978	74	1,485,031,486	547,646,223	37	1,547,000,000	484,000,000	1,063,000,000
43	Mpwawa DC	2,203,267,200	1,944,395,280	88	2,671,600,000	1,553,768,740	58	2,237,000,000	544,000,000	1,692,000,000
44	Kongwa DC	3,305,363,500	3,196,556,017	97	3,237,666,600	1,922,736,166	59	3,207,000,000	884,000,000	2,324,000,000
45	Bahi DC	1,492,761,896	1,379,542,947	92	1,435,421,896	788,307,920	55	1,700,000,000	480,000,000	1,220,000,000
46	Chamwino DC	2,478,236,000	2,148,743,370	87	2,668,678,000	741,627,903	28	2,106,000,000	576,000,000	1,529,000,000
47	Chemba DC	1,409,000,000	1,029,008,483	73	1,488,670,000	789,450,126	53	1,640,000,000	528,000,000	1,112,000,000
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>86,865,762,043</b>	<b>65,383,449,584</b>	<b>75</b>	<b>61,501,732,286</b>	<b>28,402,615,875</b>	<b>46</b>	<b>64,062,000,000</b>	<b>32,188,000,000</b>	<b>31,873,000,000</b>
	<b>Iringa</b>									
48	Iringa MC	4,027,560,000	5,617,946,074	139	5,260,707,241	2,407,842,294	46	4,357,000,000	1,195,000,000	3,162,000,000
49	Mafinga TC	3,973,479,100	4,792,659,738	121	4,613,800,100	1,904,129,717	41	4,965,000,000	1,598,000,000	3,367,000,000
50	Iringa DC	2,945,976,364	3,466,298,700	118	3,520,538,000	2,116,195,326	60	3,882,000,000	1,096,000,000	2,785,000,000
51	Mufindi DC	6,379,592,038	6,141,894,597	96	6,083,930,156	3,963,830,204	65	6,130,000,000	2,215,000,000	3,915,000,000



NA.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
52	Kililo DC	3,236,777,000	4,909,165,619	152	4,059,660,000	2,242,935,008	55	4,353,000,000	1,183,000,000	3,170,000,000
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>20,563,384,502</b>	<b>24,927,964,728</b>	<b>121</b>	<b>23,538,635,497</b>	<b>12,634,932,548</b>	<b>54</b>	<b>23,687,000,000</b>	<b>7,287,000,000</b>	<b>16,399,000,000</b>
	<b>Kigoma</b>									
53	Kigoma MC	2,644,533,284	1,653,238,965	63	2,700,496,887	1,211,896,106	45	3,000,000,000	1,106,000,000	1,894,000,000
54	Kasulu TC	1,842,706,000	1,608,102,163	87	1,931,373,000	1,156,252,923	60	2,097,000,000	612,000,000	1,485,000,000
55	Kigoma DC	698,593,970	772,320,384	111	703,870,000	457,942,232	65	719,000,000	218,000,000	501,000,000
56	Kasulu DC	2,579,576,000	2,276,868,930	88	2,791,392,790	1,372,857,440	49	2,892,000,000	848,000,000	2,045,000,000
57	Kibondo DC	1,359,724,224	1,776,512,184	131	2,563,979,600	1,651,753,224	64	2,705,000,000	674,000,000	2,031,000,000
58	Kakonko DC	791,810,460	715,700,637	90	986,119,260	539,740,132	55	1,039,000,000	260,000,000	779,000,000
59	Buhigwe DC	716,490,000	548,707,895	77	676,946,000	449,507,409	66	835,000,000	259,000,000	576,000,000
60	Uvinza DC	1,575,076,750	1,171,292,777	74	1,969,965,200	988,924,873	50	1,942,000,000	625,000,000	1,318,000,000
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>12,208,510,688</b>	<b>10,522,743,935</b>	<b>86</b>	<b>14,324,142,737</b>	<b>7,828,874,339</b>	<b>55</b>	<b>15,229,000,000</b>	<b>4,602,000,000</b>	<b>10,629,000,000</b>
	<b>Kilimanjaro</b>									
61	Moshi MC	5,429,918,203	5,754,689,855	106	6,186,836,709	3,905,564,113	63	6,460,000,000	3,083,000,000	3,377,000,000

N.A.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
62	Hai DC	3,707,763,353	2,686,219,856	72	3,730,075,404	1,953,301,596	52	3,787,000,000	750,000,000	3,037,000,000
63	Moshi DC	3,587,887,123	1,834,707,490	51	3,879,700,000	1,950,394,603	50	3,898,000,000	1,123,000,000	2,775,000,000
64	Rombo DC	1,983,430,925	1,796,827,727	91	2,034,298,097	1,092,686,125	54	2,441,000,000	749,000,000	1,692,000,000
65	Same DC	2,551,621,430	1,522,274,139	60	2,222,211,000	1,163,166,918	52	2,589,000,000	642,000,000	1,946,000,000
66	Mwanga DC	3,083,171,754	2,605,129,419	84	3,367,018,536	1,539,560,100	46	5,066,000,000	814,000,000	4,252,000,000
67	Siha DC	1,265,000,000	1,204,300,894	95	1,319,603,000	510,464,570	39	1,532,000,000	456,000,000	1,076,000,000
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>21,608,792,788</b>	<b>17,404,149,380</b>	<b>81</b>	<b>22,739,742,746</b>	<b>12,115,138,025</b>	<b>53</b>	<b>25,773,000,000</b>	<b>7,617,000,000</b>	<b>18,155,000,000</b>
	<b>Lindi</b>									
68	Lindi MC	2,500,000,000	1,661,094,101	66	2,447,320,000	1,190,559,799	49	2,850,000,000	879,000,000	1,971,000,000
69	Nachingwea DC	3,281,305,738	3,174,253,598	97	4,088,132,973	3,151,225,355	77	4,002,000,000	1,033,000,000	2,969,000,000
70	Kilwa DC	4,647,511,800	4,667,351,052	100	4,637,321,504	3,140,562,431	68	5,500,000,000	1,601,000,000	3,899,000,000
71	Liwale DC	3,322,204,936	2,742,795,782	83	3,850,244,936	2,026,593,992	53	3,854,000,000	1,001,000,000	2,854,000,000
72	Mtama DC	2,201,075,716	1,846,082,079	84	4,253,369,335	1,102,973,118	26	2,744,000,000	668,000,000	2,076,000,000
73	Ruangwa DC	3,034,624,900	3,369,772,006	111	4,801,866,300	3,108,259,342	65	4,961,000,000	1,476,000,000	3,485,000,000

N.A.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
	Jumlia ndogo	18,986,723,090	17,461,348,618	92	24,078,255,048	13,720,174,036	57	23,911,000,000	6,658,000,000	17,254,000,000
	Mara									
74	Musoma MC	2,131,421,000	2,023,484,408	95	2,681,703,943	1,695,877,042	63	2,939,000,000	670,000,000	2,269,000,000
75	Tarime TC	1,249,643,870	1,549,522,969	124	1,777,985,886	1,002,827,070	56	1,550,000,000	363,000,000	1,187,000,000
76	Bundia TC	1,150,000,000	1,243,165,894	108	1,377,381,380	892,383,333	65	1,459,000,000	453,000,000	1,006,000,000
77	Bundia DC	1,406,368,400	1,057,064,514	75	1,426,548,000	721,061,024	51	1,776,000,000	599,000,000	1,177,000,000
78	Musoma DC	1,441,892,000	1,527,946,291	106	1,740,936,236	821,667,073	47	1,750,000,000	552,000,000	1,198,000,000
79	Serengeti DC	3,422,352,000	2,950,337,365	86	3,277,872,000	1,117,246,919	34	3,558,000,000	980,000,000	2,578,000,000
80	Tarime DC	4,811,880,000	5,044,196,940	105	6,169,019,812	5,196,910,508	84	7,214,000,000	2,448,000,000	4,766,000,000
81	Rorya DC	1,350,378,000	956,637,757	71	1,350,378,000	626,775,226	46	1,380,000,000	399,000,000	981,000,000
82	Butiama DC	1,333,761,000	982,195,540	74	1,522,500,000	666,830,934	44	1,545,000,000	469,000,000	1,076,000,000
	Jumlia ndogo	18,297,696,270	17,334,551,678	95	21,324,325,257	12,741,579,128	60	23,171,000,000	6,933,000,000	16,238,000,000
	Mbeya									
83	Mbeya CC	12,736,800,000	12,934,934,265	102	15,949,287,599	9,438,441,645	59	16,610,000,000	7,222,000,000	9,389,000,000

N.A.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwezi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
84	Chunya DC	4,398,634,260	3,519,929,242	80	5,258,459,289	2,602,895,821	49	4,847,000,000	1,576,000,000	3,270,000,000
85	Kyela DC	4,230,711,000	3,439,597,667	81	3,621,066,676	2,111,508,726	58	3,884,000,000	1,053,000,000	2,831,000,000
86	Mbeya DC	3,839,572,000	3,813,232,539	99	3,888,212,000	2,057,466,702	53	4,373,000,000	1,444,000,000	2,929,000,000
87	Rungwe DC	5,371,120,000	3,979,488,164	74	5,331,574,763	3,599,171,247	68	5,306,000,000	1,337,000,000	3,969,000,000
88	Mbarali DC	4,363,850,000	3,909,012,680	90	4,672,006,000	2,586,821,861	55	4,790,000,000	1,740,000,000	3,050,000,000
89	Busokelo DC	2,192,698,000	1,763,943,771	80	1,523,020,000	1,073,893,679	71	1,594,000,000	378,000,000	1,216,000,000
	<b>Jumlia ndogo</b>	<b>37,133,585,260</b>	<b>33,360,138,328</b>	<b>90</b>	<b>40,243,626,327</b>	<b>23,470,199,681</b>	<b>58</b>	<b>41,404,000,000</b>	<b>14,750,000,000</b>	<b>26,654,000,000</b>
	<b>Songwe</b>									
90	Tunduma TC	4,554,643,000	5,493,777,173	121	5,374,771,500	3,766,062,593	70	5,636,000,000	2,089,000,000	3,547,000,000
91	Momba DC	1,332,651,550	683,460,433	51	1,346,500,000	1,265,175,052	94	1,586,000,000	559,000,000	1,026,000,000
92	Mbozi DC	3,423,111,775	3,971,373,986	116	3,675,217,496	2,601,482,757	71	3,047,000,000	1,090,000,000	1,957,000,000
93	Ileje DC	1,057,547,000	774,840,707	73	1,233,751,156	699,833,389	57	1,403,000,000	338,000,000	1,064,000,000
94	Songwe DC	3,525,054,071	2,637,244,615	75	2,933,015,389	1,450,028,615	49	3,150,000,000	1,107,000,000	2,043,000,000
	<b>Jumlia ndogo</b>	<b>13,893,007,396</b>	<b>13,560,696,914</b>	<b>98</b>	<b>14,563,255,541</b>	<b>9,782,582,406</b>	<b>67</b>	<b>14,822,000,000</b>	<b>5,183,000,000</b>	<b>9,637,000,000</b>

N.A.	Mkoa/ Halmashauri	2019/20			2020/21			Makisio ya Mwaka wa fedha 2021/22		
		Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi (TZS)	%	Makisio yaliyodhinishwa (TZS)	Mapato halisi hadi Mwazi Februari, 2021 (TZS)	%	Jumla ya makisio (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Maendeleo (TZS)	Makisio ya Matumizi ya Kawaida (TZS)
	<b>Morogoro</b>									
95	Morogoro MC	6,705,926,213	7,525,668,625	112	8,478,799,218	4,612,045,613	54	11,504,000,000	5,813,000,000	5,690,000,000
96	Ifakara TC	2,909,994,900	1,863,800,265	64	3,089,729,000	1,857,799,990	60	3,927,000,000	1,312,000,000	2,615,000,000
97	Morogoro DC	2,201,584,000	1,749,675,074	79	2,728,732,000	1,836,261,112	67	3,026,000,000	967,000,000	2,059,000,000
98	Kilosa DC	5,296,079,600	3,847,927,184	73	5,227,499,212	2,416,790,877	46	5,240,000,000	1,632,000,000	3,608,000,000
99	Mlimba DC	4,197,110,580	4,097,233,343	98	4,778,836,847	1,696,274,976	35	3,367,000,000	1,100,000,000	2,267,000,000
100	Ujanga DC	2,877,250,000	2,770,548,823	96	2,821,852,200	1,642,782,433	58	2,432,000,000	764,000,000	1,668,000,000
101	Mvomero DC	4,118,680,628	2,758,490,426	67	3,198,735,187	1,884,255,276	59	3,596,000,000	1,140,000,000	2,456,000,000
102	Gairo DC	1,018,832,700	754,327,790	74	1,092,495,288	473,436,286	43	1,220,000,000	292,000,000	928,000,000
